SportPesa
TZS. 450,150,500
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**MAHOJIANO MAALUM**
Msimamo CHADEMA tozo miamala ya simu
UKURASA 4


DARASSA
Nipashe BT BURUDANI TELE
NANCY SUMARI
Tuipe muda Miss Tanzania itarudi imara kama zamani

UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Agosti 28, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580686
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mauaji mengine askari wawili Dar

UKURASA 2

## IGP atoa onyo kali miili polisi waliouawa ikiagwa

Mwili wa aliyehusika wakabidhiwa kwa ndugu ... *Endelea ukurasa 2*





Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene na Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, wakiaga miili ya askari polisi wanne waliouawa na mtu mwenye silaha, kwenye viwanja vya gwaride wa Polisi Barracks, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## Jerry Silaa asalimika kutiwa pingu

UKURASA 3

Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa, akiwa ameketi mapema ukumbini akisubiri kuhojiwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, bungeni jijini Dodoma jana. Juzi kamati hiyo iliviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kumkamata na kumfikisha mbele ya kamati baada ya kushindwa kuripoti mwenyewe. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UKURASA WA 3

## MAHAKAMA YARIDHIA KIFUNGO CHA MAISHA BABA KUBAKA MTOTO



MAHAKAMA ya Rufani Tanzania imebariki Simon Emmanuel kuendelea kutumikia kifungo cha maisha jela kwa...

MICHEZO MTIBWA ITANIRUDISHA SIMBA KWA KISHINDO - AME UK.23
MAONI, KATUNI UK.6

# Mauaji mengine ya askari Dar

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia Mohamed Jumaa (37), maarufu kama Lardh JM, mkazi wa Kariakoo, kwa tuhuma za mauaji ya walinzi wawili na kujeruhi wengine sita.

Kamanda wa Kanda hiyo, Muliro Jumanne, aliwataja waliouwawa kuwa ni mlinzi wa kampuni ya ulinzi ya Lock Fort, Eliakimu Moro na Sanko Bakari ambaye ni mlinzi binafsi, mkazi wa Buguruni.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi jioni saa 12:00 maeneo ya Tungi wilayani Kigamboni katika kituo cha mafuta cha JM.

"Mtuhumiwa aliwaua walinzi hao kwa kuwagonga kwa makusudi na gari lenye namba T 176 CVP aina ya Leyland DAF lori, lililokuwa na tela ambalo halina namba za usajili," alisema.

Muliro alisema mtuhumiwa huyo alifika katika kituo hicho cha mafuta alichokuwa anakimiliki, kwa ajili ya kuhamisha mali zake, lakini alichukua gari lake na kutoka nje ya kituo.

Alisema ghafla alirudi nalo kwa kasi huku likiwa halina tela na kuwagonga walinzi hao waliokuwa getini na kufariki dunia papo hapo na kujeruhi watu wengine sita.

"Mohamed alikwenda eneo lile ambalo tayari alikuwa ameshakabidhiwa na benki na baadae aliingia mtuhumiwa akadai anachukua lori lake, alipochukua alitoka nalo nje. Baada ya muda, lori lilirudi kwa kasi wakati walinzi wakiwa wamefunga mlango wa geti na kuingia ndani kwa nguvu na kusababisha vifo vya walinzi hao."

"Mtuhumiwa huyu alikuwa na kesi ya madai Mahakama Kuu yenye namba 118/2018 iliyofunguliwa na benki ya Access baada ya kushindwa kulipa mkopo kwa muda mwafaka aliochukua katika benki hiyo.

Alisema aliyeshinda zabuni hiyo alikuwa Fahad Mohamed ambaye ndiye aliyetoa taarifa polisi baada ya tukio hilo kutokea eneo hilo.

Kamanda alisema mtuhumiwa huyo alishindwa mahakamani licha ya kukata rufani mara kadhaa na hatimaye mahakama ilitoa amri ya kuuzwa kwa kituo hicho.

Kamanda Muliro alisema wanaendelea na uchunguzi kuhusiana na tukio hilo.




Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Sheikh Khamis Mataka, akizungumza wakati wa mkutano wa viongozi wa dini uliojadili kutoa maoni juu ya sheria ya bima ya afya, ulioandaliwa na Policy Forum, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# IGP atoa kauli kali miili polisi ikiagwa

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, amesema mauaji dhidi ya askari wanne yaliyofanywa jijini Dar es Salaam Jumatano, yanapaswa kuwa funzo kwa askari wa jeshi hilo kutocheza na mtu wa ovyo na wasimwamini kila wanayemwona.

IGP Sirro alitoa kauli hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa mazishi ya askari hao wanne yaliyofanyika Viwanja vya Polisi Kilwa.

"Matukio kama haya yanapotokea askari wana kitu cha kujifunza, wananchi wana kitu cha kujifunza, wafiwa wana kitu cha kujifunza.

"Watanzania ukishakuwa na mtoto mhalifu, mtoto mwizi, mtoto gaidi, mwenye tabia mbaya mbaya, usiposhirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama maana yake kuna mawili, moja; anaweza kuleta madhara kwa Watanzania. La pili; anaweza mwenyewe uhai wake akaupoteza," alionya.

IGP Sirro alisema Hamza (kijana aliyetekeleza mauaji hayo), kama ndugu zake wangewajibika vizuri, wasingekuwa huko kuaga miili ya askari hao.

"Tungetegemea Watanzania uzae mtoto kesho anakuwa waziri, IGP, mwalimu, lakini ukizaa mtoto akawa mwizi, karuanja ni tatizo kwako na kwa Watanzania," alisema.

Alifafanua kuwa wafiwa kupitia tukio hilo, lipo la kujifunza kuwa askari hao hawakuwa magaidi, wezi, majambazi, lakini wamekufa wakiwalinda, hivyo vifo vyao ni heshima kwao.

"Tusipate huzuni sana, tuwaombee kwa sababu walichokuwa wanafanya ni kuwatetea Watanzania. Kwa ofisa polisi na viongozi wa upande wa vyombo vya ulinzi na usalama, kuna kitu cha kujifunza kwa kuwa askari wetu kufa kwa risasi kwa kupigwa risasi kichwani.

"Huwa ninawaambia siku zote, usicheze na mtu wa ovyo ovyo, usimwamini kila mtu, hii yote ni kwa sababu ya imani walipomwona huyu mtu wa ovyo ovyo Hamza anawasogelea, walijua ni Mtanzania wa kawaida, kumbe alikuwa na pistol akafanya alichofanya," alisema.

IGP Sirro aliwaonya askari kuwa wakizubaa wasililaumu Jeshi la Polisi wala serikali kwa sababu wana mafunzo ya kutosha.

"Ni kipindi kigumu kwamba tuna changamoto siyo kila mtu ni rafiki, kama jeshi tumepoteza vijana wadogo sana, sisi tunaokaribia kustaafu tulitegemea wangeendesha jeshi lakini kwa sababu ni sehemu ya maisha yetu ninaamini wale mliobaki mnajifunza sasa.

"Siyo kila mtu anapenda askari polisi, siyo kila mtu anapenda vyombo vya dola, wakati mwingine tunaambiwa tunatumia nguvu au hatutendi haki lakini yanapotokea haya huwa hatusikii watu wakizungumzia haki ya polisi.

"Maana yake nini? Tusiwe na 'double standard', kazi hii ni ngumu sana, mtu akiona hivi anaona ni kazi rahisi, lakini kupambana na mhalifu siyo jambo dogo," alisisitiza.

IGP Sirro aliwahakikishia wafiwa kuwa Jeshi la Polisi litahakikisha vijana hao waliofariki dunia wanapata haki zao.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema vijana hao wamekufa kishujaa.

Alitoa salamu za Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Simbachawene alisema msiba huo una mambo ya kujifunza kwamba unapokuwa askari lazima uwe tayari wakati wote.

"Ninadhani IGP tukubali tumeumia na tumeumizwa lakini na sisi tunapochukua hatua za awali za kupambana na uhalifu, tusipambane kizamani ili tuokoe watu wengi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akizungumza kwa niaba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, alikabidhi kwa IGP Sirro Sh. milioni sita kama rambirambi ili zigawiwe kwa ndugu wa marehemu hao.

HABARI KITAIFA

# Jerry Silaa asalimika kupigwa pingu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Ukonga (CCM), Jerry Silaa, amejipeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge baada ya juzi kutotii wito wa kuhojiwa kwa mara ya pili.

Kutokana na kushindwa kufika kuhojiwa tena, kamati iliagiza akamatwe na kufikishwa jana saa 4:00 asubuhi.

Silaa alitinga jana katika viwanja vya bunge mapema kabla ya muda uliokuwa umepangwa na Kamati hiyo na kupitia geti la Waziri Mkuu tofauti na geti kubwa la kuingilia wabunge, akiwa amebeba begi dogo la mkononi na chupa ya maji.

Baada ya kuingia kwenye viwanja vya bunge, Silaa aliendelea na shughuli zingine ndani ya jengo la utawala na kuingia ukumbini ilipofika saa 3:50 asubuhi kabla ya Mwenyekiti wa Kamati, Emmanuel Mwakasaka, na wajumbe wake kuingia saa 4:00 asubuhi.

Hata hivyo, baada ya mwenyekiti huyo kuingia na wajumbe, mbunge huyo alitakiwa kupisha kwanza kamati na baadaye kuitwa saa 5:00 asubuhi.

Mwenyekiti Mwakasaka aliwaambia waandishi kuwa Silaa amefika kwa ajili ya kuendelea na shauri lake na kamati hiyo ilikamilisha kumhoji saa 5:37 asubuhi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukamilisha mahojiano hayo, Mwakasaka alisema kamati ilikuwa inakamilisha shauri la pili la Silaa na amefika kufanya mahojiano.

"Tumekamilisha mashauri yote mawili kwa ukamilifu la Silaa na Askofu Josephat Gwajima," alisema.

Alipoulizwa kuhusu sababu za kutofika mbele ya kamati juzi na kuagiza akamatwe, Mwakasaka alisema: "Sisi nia yetu ilikuwa yeye kufika mbele ya kamati na amefika leo (jana). Sasa yale ambayo amejibu kwa nini hakufika jana ni moja ya vitu ambavyo kamati inaendelea kuvifanyia kazi."

"Hata unapoahirisha kesi mahakamani hupewi tena barua ya wito. Kama ulipewa leo kesi ikaahirishwa hata mahakama za kawaida ikaahirishwa kesi hadi kesho, hautolewi wito tena. Kwa hiyo yeye alikuwa na taarifa. Kamati si kazi yake kumtafuta mtu bali anapaswa kufika kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo," aliongeza.

Awali, Silaa alipoulizwa sababu za kutofika alisema: "Mimi nilihojiwa Jumanne na kuwasilisha utetezi wangu na kila nyaraka iliyopaswa kuwasilishwa. Siku hiyo nilikuwa nimefiwa kama ningeomba udhuru sidhani kama ningekubaliwa. "Kwa picha ninayoiona hapa sidhani kama wangenielewa. Kwa hiyo jana nilikuwa na matatizo ya kiafya na nilikuwa najiandaa kwenda mazikoni Arusha lakini kama watu wengine nikaona kwenye mitandao lakini sikutafutwa na polisi. Niliamua kufika mwenyewe hapa na Nipashe ni mashahidi."

Pia alisema hakufika kutokana na kutopewa barua ya wito.

Juzi, kamati hiyo ilimwomba Spika wa Bunge, Job Ndugai, kutoa kibali cha kukamatwa mbunge huyo na kumfikisha mbele ya kamati jana saa 4:00 asubuhi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, alisema shahidi huyo alipaswa kufika mbele ya kamati hiyo tena juzi saa tano asubuhi lakini hakufika na hakutoa taarifa yoyote ya sababu za kutofanya hivyo.

Agosti 23, mwaka huu, Silaa aliitwa kwa mara ya kwanza mbele ya kamati hiyo kutokana na wito wa Spika wa Bunge kutokana na tuhuma mbalimbali zinazomkabili ikiwamo madai ya kusema uongo na kushusha hadhi na heshima ya bunge.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wakuu wa mikoa ya Tabora, Dk. Batilda Burian (kulia) na Katavi, Mwananvua Mrindoko (katikati) baada ya kuwasili kweye daraja la Koga linalotenganisha mikoa hiyo kukagua daraja hilo ambalo ujenzi wake umekamilika, jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU.**

# Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar yazidiwa corona

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

HOSPITAL ya Mnazi mmoja Zanzibar, inakabiliwa na upungufu wa gesi ya Oksijeni kutokana na kuelemewa na wagonjwa wa corona wanaohitaji kuwekewa gesi hiyo ili kuwasaidia kupumua.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Hospital hiyo, Hassan Makame, alisema hali sio shwari hospitalini huko kutokana na kuwa na wagonjwa wengi wa corona na kuna upungufu mkubwa wa mitungi ya Oksijeni.

"Tumetuma watu wetu Dar es Saalam kwenda kuchukua gesi, kuna baadhi ya wagonjwa wanatumia zaidi ya mitungi miwili kwa siku," alisema.

Kiongozi huyo alisema wanahitaji zaidi ya mitungi 300 kwa siku tano, hivyo wanahitaji mitungi ya akiba kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa hospitalini huko.

Alisema kwa muda aliokuwa anazungumza na waandishi wa habari jana, walikuwa na mitungi 180, ambayo ni kidogo kulinganishwa na kiwango cha wagonjwa wanaohitaji mitungi ya gesi kuokoa uhai wao.

"Kuna baadhi ya wagonjwa wa corona hawawezi kuishi bila ya kupata Oksijeni, ninawashauri wananchi wachukue tahadhari corona na kufuata miongozo ya wataalamu wa afya kwa sababu corona ipo na inaathiri sana," alihadharisha.

Alisema wagonjwa hao wametengewa wodi maalum hospitalini huko ili kuepusha maambukizi kwa wagonjwa wengine waliopo.

Akizungumzia kuhusu maiti za watu waliofariki dunia kwa corona, katibu huyo alisema zinakabidhiwa jamaa zao kwa ajili ya mazishi lakini hupewa utaratibu wa kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo. Nipashe ilimtafuta Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, ambaye alikiri kuwapo kwa uhaba wa gesi hospitalini huko na kusema kuwa wanafanya jitihada kuagiza gesi.

Alisema wagonjwa walioko hospitalini huko ni 36 na tayari watu 40 wameshafariki dunia kutokana na corona.

Waziri huyo alisema wanatarajia kufungua kambi maalum ya wagonjwa wa corona katika Kituo cha Afya Fuoni Kibondeni endapo idadi ya wagonjwa itaongezeka.

Aliwataka wananchi kuchanja chanjo ya corona kwa sababu waliopata ugonjwa huo, hakuna aliyepata chanjo.

Kwa mujibu wa taarifa ya waziri huyo ya Agosti 12, mwaka huu, Zanzibar ilikuwa na wagonjwa wa corona 390 na vifo 15.

Waziri Mazrui alisema kati ya hao 390 waliopata corona, Watanzania walikuwa 112 na wageni 278.

## Mahakama yaridhia kifungo cha maisha baba kubaka mtoto

**NA KULWA MZEE**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania imebariki Simon Emmanuel kuendelea kutumikia kifungo cha maisha jela kwa kumbaka mtoto wa kambo baada ya kuona sababu alizotoa kupinga adhabu hazina msingi.

Hukumu hiyo ilitolewa jana mbele ya jopo la majaji watatu, Stella Mugasha, Ignas Kitusi na Lilian Mashaka baada ya kupitia hoja za pande zote mbili.

Mlalamikaji alitiwa hatiani na Mahakama ya Wilaya ya Kahama kwa kosa la kumbaka binti wa miaka minane na kuhukumiwa kifungo cha maisha jela.

Tukio linadaiwa kutokea Januari 30, 2009 katika Kijiji cha Nyandekwa saa kumi jioni. Mlalamikaji anadaiwa alirudi nyumbani 10:00 akamtuma binti akafuate karatasi kitandani kwake ili afungie tumbaku.

Mtoto alifuata makaratasi lakini hakuyaona na mlalamikaji aliingia chumbani akamlaza kitandani huku akimbana miguu na kumbaka. Kutokana na kitwendo hicho, mtoto alilia kuomba msaada lakini hakukuwa na watu wa kumsaidia.

Inadaiwa mama wa mtoto alikwenda kwenye biashara, aliporudi saa 12:00 jioni alimkuta binti yake akilia na alikuwa akitokwa damu na nguo zilikuwa zimechafuka kwa damu.

Mama ambaye ni shahidi wa pili, anadaiwa alimwuliza binti yake akamfahamisha tukio lote na kubaini mlalamikaji alimbaka mtoto ndipo alipokwenda kuripoti Polisi.

Mlalamikaji alikana kufanya tukio hilo lakini alikubali kuwa shahidi wa pili ni mkewe na shahidi wa kwanza ni mtoto wake wa kambo.

Katika rufani, mlalamikaji alijiwakilisha mwenyewe na upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wampumbulya Shani.

Mlalamikaji alitoa sababu mbalimbali kupinga adhabu ya kifungo cha maisha, alidai Jaji wa Mahakama Kuu Shinyanga alikosea kuitupa rufani yake ya kupinga hukumu ya Mahakama ya Wilaya Kahama kwa kuangalia ushahidi wa familia. Pia aidai kuwa ushahidi uliokuwapo kwenye kumbukumbu za mahakama ni dhaifu.

Akijibu hoja hizo, Wakili Shani alidai sababu za kupinga adhabu alizotoa mlalamikaji ni mpya na hakuzitoa Mahakama Kuu.

Jamhuri iliomba rufani itupwe kwa kuwa walithibitisha shtaka dhidi ya mshtakiwa bila kuacha shaka yoyote.

Katika uamuzi wao, majaji hao walikubaliana na hoja za Jamhuri kwamba shahidi wa kwanza ambaye ni mtoto na shahidi wa pili ambaye ni mama, ushahidi wao umethibitisha kosa dhidi ya mlalamikaji.

## MAHOJIANO MAALUM

# Msimamo CHADEMA tozo za miamala ya simu

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI tozo za miamala ya simu zikiendelea kuibua mjadala wa kitaifa, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetoa msimamo wake kuhusu suala hilo.

Tozo hizo zilizoripotiwa kuingizia serikali mapato ya Sh. bilioni 48 katika mwezi wa kwanza tangu kuanza kutozwa kwake, zimekuwa zikilalamikiwa na wadau mbalimbali wakiwamo wananchi wa kawaida.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, ni miongoni mwa viongozi wakuu waliojitokeza hadharani kuzungumzia tozo hizo, msimamo wake ukiwa 'Bunge lilikuwa na nia njema kupitisha sheria ya kuanzisha tozo hizo, ili kupata fedha zitakazotumika kutekeleza miradi ya maendeleo'.

Katika mazungumzo mahususi na Nipashe mkoani Dar es Salaam juzi, Katibu Mkuu wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), Catherine Ruge, alisema chama hicho hakiungi mkono tozo hizo.

Alisema ufuatiliaji wa chama hicho kuhusu tozo hizo, umebaini zimekuwa chungu kwa wanawake, hasa wanaoishi vijijini ambao kwa kiwango kikubwa wanategemea miamala ya simu katika kuendesha shughuli zao za kiuchumi, vikiwamo vikundi vyao vya kuweka akiba (vikoba).

Catherine alisema BAWACHA ikipata fursa ya kukutana na kuzungumza na Rais Samia Suluhu Hassan, itamshauri azifute tozo hizo.

Mbali na tozo za miamala ya simu, Catherine katika mazungumzo na Nipashe, pia alizungumzia chanjo ya corona inayoendelea kutolewa nchini, hali ya kisiasa nchini na maendeleo ya BAWACHA katika kipindi hiki ambacho CHADEMA imekuwa na mvutano na uongozi wa Bunge kuhusu uteuzi wa wabunge wa viti maalum kupitia chama hicho.

Ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo hayo ya Nipashe na kiongozi huyo wa CHADEMA:

**SWALI: Kuna kilio kinasikika dhidi ya tozo za miamala ya simu. Ni upi msimamo wa BAWACHA kuhusu suala hili?**

**CATHERINE:** Bawacha imepokea jambo hili kwa masikitiko kwani ni jambo ambalo linawaumiza sana wanawake na hasa wanaoishi vijijini.



Catherine Ruge, **PICHA: MAKTABA**

Miamala ya simu ilikuwa imewezesha vikundi vya kinamama, yaani vikoba, kukusanya na kutuma michango yao kwa njia ya mtandao, hivyo kuwafanya kuwe na usalama zaidi wa fedha zao.

Kwa sasa hawawezi kufanya hivyo kwani tozo hizo ni kubwa na zinakatwa kwa anayetuma na anayepokea.

Aidha, wanawake vijijini ambao walikuwa wanategemea kupokea fedha kutoka kwa watoto au ndugu walioko mbali, wanashindwa kupokea hizo fedha na hivyo kufanya jitihada za kupambana na umaskini kurudi nyuma sana hasa huko vijijini na hata mijini.

Leo tozo hizi hata ukituma mchango wa matibabu au rambirambi unakatwa fedha nyingi, wanawake wajasiriamali wanaendelea kuumizwa na tozo hizi.

**SWALI: CHADEMA kupitia kwa Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, imeshaweka wazi msimamo wake wa kuunga mkono kutolewa kwa chanjo ya corona nchini. Je, BAWACHA mnashiriki vipi kuhamasisha wananchi kuchanja?**

**CATHERINE:** Baraza linaunga mkono suala la chanjo na hata mimi binafsi nimeshapata chanjo na ninawahimiza wanawake wote nchini kujitokeza kwa hiari yao kwenda kupata chanjo, kwa ajili ya kulinda uhai wao na watoto wao.

**SWALI: Uongozi wa chama umewafuta uanachama baadhi ya viongozi, akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wenu, Halima Mdee. Uamuzi huu umeliathiri vipi baraza?**

**CATHERINE:** Baraza liko imara sana na linaendelea na ajenda yake kuu, kwa sasa ya kudai Tume huru ya Uchaguzi, ili kutoa fursa kwa wanawake wengi kushiriki uchaguzi ulio huru na haki.

Tunaendelea kuwaunganisha wanawake wote nchini kuhakikisha kuwa viongozi watakaochaguliwa wanakuwa wamepatikana kwa njia za kidemokrasia na watakuwa watetezi wa kweli wa wananchi na hawataenda kutunga sheria za kuwaumiza kama hizi tozo na mengineyo.

**SWALI: Ukipata dakika moja leo kuteta na Rais Samia, utamwambia nini kwa manufaa ya taifa?**

**CATHERINEl:** Kwanza; BAWACHA tutampongeza kwa kuweka historia katika nchi yetu kwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke.

Pili; tutamweleza matatizo ambayo yanaikabili nchi yetu na hasa yanayotokana na kukosekana kwa Katiba nzuri na ambayo imezaa sheria mbaya zinazokandamiza haki, uhuru na hususani haki za wanawake.

Tutamweleza pia kuhusu sheria mbaya na kandamizi ikiwamo Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, wanawake wenye watoto wanapokuwa gerezani na watoto wao wanakosa fursa za kupata malezi bora na elimu.

Mama akifungwa akiwa na mtoto, huyo mtoto naye anakuwa mfungwa. Ni jambo linalohitaji kufanyiwa marekebisho, ili watoto wetu wasihukumiwe bila kutenda makosa yoyote na maisha yao yanaanza kuharibika.

Tutamweleza kuhusu watoto wa kike ambao wananyimwa fursa ya kwenda shule, kwa sababu za ujauzito na haki ya watoto wa kike kupata taulo za kike kwa bei nafuu na hii inawezekana kwa kuondoa kodi na tozo kwenye taulo hizo.

Nikikutana na Rais Samia, nitamweleza pia kuhusu changamoto za wanawake nchini katika masuala ya uchumi, afya, elimu na maji.

Nitamweleza Rais kuhusu kinachoendelea dhidi ya Mwenyekiti wetu, Freeman Mbowe, na kumshauri atumie mamlaka yake amtake DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka) afute kesi hiyo kwa kuzingatia Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 kifungu cha 29 (6) kulifuta shauri hilo.

**SWALI: Unaizungumziaje hali ya kisiasa iliyopo nchini kwa sasa?**

**CATHERINE:** Hali ni mbaya kwa sababu watu wananyimwa uhuru wa kukusanyika, kutoa maoni, kushiriki shughuli za siasa, kufanya makongamano ya kisiasa na kadhalika.

Polisi wanawanyanyasa wanawake wanaojihusisha na shughuli za kisiasa kwani wanawakamata na kuwadhalilisha na mfano ni mimi mwenyewe.

Niliwekwa ndani polisi na kunyimwa hata haki ya kubadilisha nguo, kupata sanitary pads (taulo za kike) kwa zaidi ya siku tano. Huu sio tu kwamba ni udhalilishaji, bali ni ukatili uliopitiliza dhidi ya wanawake. Wanawake wataendelea kudai Katiba Mpya na Tume huru ya Uchaguzi nchini.

■ ***Imeandaliwa na Haika Christopher (SJMC), Leyla Joho (TUDARCo) na Sechellah Nakamba (SJMC).***

---

# PASS yadhamini bilioni 13.5/- kwa usindikaji korosho

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

TAASISI ya Uwezeshaji Sekta ya Kilimo (PASS Trust) imedhamini mikopo ya zaidi ya Sh. bilioni 13.5 kwa wasindikaji wadogo, wanunuzi wa korosho na waagizaji wa pembejeo kwa mwaka huu pekee.

Mkurugenzi Mtendaji wa PASS Trust, Yohane Kaduma, alibainisha hayo jana mjini Mtwara alipozungumza kwenye kongamano la wadau wa korosho.

Alisema katika kipindi hicho, taasisi hiyo imedhamini Sh. milioni 231 kwa wasindikaji wadogo wa korosho, Sh. bilioni 2.3 kwa wanunuzi wa korosho na bilioni 10.97, kwa waagizaji wa pembejeo.

"Na mchakato unaendelea kwa maombi ya Sh. bilioni 23.5, kwa ajili ya waagizaji wa pembejeo na vifungashio vya korosho," alisema Kaduma na kuongeza:

"Katika kuhakikisha tunadhamini mnyororo mzima wa zao la korosho kwa msimu wa mwaka huu tumejiwekea malengo ya kuwafikia wanunuzi na wasindikaji wapatao 70, ambapo kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 27 zitadhaminiwa.

"PASS Trust imekuwa ikifanya kazi na taasisi za fedha zikiwamo benki za CRDB, BOA, Equity, NMB, NBC na TADB ambazo tumefanya kazi kwa ukaribu katika kuhakikisha wakulima na wadau wa kilimo katika kanda hii ya kusini wanapata mikopo kupitia udhamini wa PASS."

Alisema vikwazo vya mitaji miongoni mwa wakulima bado vipo na vitazidi kuwapo, hivyo ipo haja ya kuomba taasisi zingine zaidi za fedha kuangalia jinsi ya kuongeza kiwango cha fedha zinazotengwa, kwa ajili ya mikopo ya kilimo.

"Niwasihi wenzetu wa taasisi za fedha kupuuzia dhana kwamba kilimo 'hakibenkiki' ili tuungane katika kuinua na kuboresha maisha ya Watanzania kupitia upatikanaji wa mikopo ya kilimo," alisema.

Kaduma aliwataka wakulima kuhakikisha mikopo inarejeshwa, ili watoaji wa mikopo hiyo waendelee kuwawezesha na kuwainua wakulima wengine wadogo wasio na uwezo wa kupata fedha.

## TANGAZO




betPawa inatoa nafasi kwa wateja wote kuanza msimu mpya wa Ligi kuu ya Uingereza wakiwa na gari mpya.

Mtanzania mmoja atabahatika kujishindia Toyota RAV4 mpya kabisa. Watano watajishindia PS5 na CD ya Fifa 21, na wawili watapata shilingi laki 5 kila mmoja kwa ajili ya shopping Shoppers supermarket.

Tumia nafasi yako kushinda kikubwa ZAIDI, bashiri mechi yoyote ya ligi kuu Uingereza kupitia betPawa na uingie katika droo.

Una nafasi hadi Jumapili ya tarehe 29 Agosti kushiriki na washindi 8 watapatikana katika droo siku ya Jumatatu tarehe 30 Agosti.

Wataalikwa Dar es Salaam katika shindano la upigaji penalti mwezi Septemba.
Mshindi ataondoka na Toyota RAV4, na hakuna mtu ataondoka bila zawadi.

Je utakua mshindi? Unaweza kushiriki kwa kubashiri kwa kiwango kidogo cha TSH 1 tu.

Tukutane sheli na betPawa!
Ingia **betpawa.co.tz/epl-launch-giveaway**

betPawa

Cheza kiasi. 18+. betPawa imesajiliwa chini ya bodi ya michezo ya kubashiri ya Tanzania. Leseni #SBI000000026.

216428702

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu, wachezaji umakini unahitajika dirisha la usajili

**KLABU** za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili, bado zipo mawindoni, kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao kuelekea msimu mpya wa 2021/22, unaotarajiwa kuanza mapema mwishoni wa mwezi ujao.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), dirisha la usajili msimu huu litafungwa rasmi Jumanne ijao, Agosti 31, saa sita usiku tayari kwa msimu mpya unaotarajiwa kuanza Septemba 26, mwaka huu kwa upande wa Ligi Kuu Bara.

Kuelekea kufungwa kwa dirisha hilo, tunazipongeza klabu, ambazo tayari zimetangaza mapema wachezaji isiyowahitaji kwa msimu mpya, hivyo kuwapa nafasi ya kutafuta timu nyingine kabla ya dirisha hilo kufungwa mwishoni mwa mwezi huu.

Hata hivyo, wakati huu klabu zikiendelea kufanya usajili, hazina budi kuzingatia kanuni, huku wachezaji nao wakiongeza umakini kwa kuzingatia kwenda kulinda vipaji vyao kwa timu zinazowasajili.

Hatutarajii kuona baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili, kunaibuka mvutano kwa klabu moja kukata rufaa ya kupinga mchezaji wao kusajiliwa na klabu kinyume cha taratibu wakati akiwa na mkataba na mwajiri wake wa mwanzo.

Tunatoa tahadhari hiyo mapema kutokana na kutambua kwamba tayari kumeanza mvutano wa chini kwa chini kwa Klabu ya Kagera Sugar kueleza kutotambua usajili wa mshambuliaji wao, Yusuph Mhilu kwenda Simba kwa kwa kile inachodai taratibu hatokufuatwa.

Tunatambua huenda haitakuwa kwa Kagera Sugar na Simba pekee, kwani huenda baada ya dirisha la usajili kufungwa kukaibuka madudu mengi kama hayo na hivyo klabu kukatiana rufaa zikipinga wachezaji wao kusajiliwa kinyume cha taratibu.

Hivyo, wakati huu zikiwa zimebaki siku nne kabla ya dirisha hilo kufungwa, tunataka kuona kasoro ambazo zinaweza kufanyiwa kazi mapema kwa klabu na wachezaji kufuata taratibu, kutekelezwa mapema, ili kuepuka baadaye kupoteza muda na gharama za kukata rufaa.

Katika hilo pia, wachezaji hawana budi kuheshimu mikataba yao na kama ni suala la kuhama, kufuata taratibu husika, ili kutoleta mvutano dirisha la usajili litakapofungwa.


Pia, wachezaji wanaohama kutoka klabu moja kwenda nyingine pamoja na kuzingatia maslahi yao, hawana budi kumulika zaidi kujiunga na timu watakazokwenda kupata nafasi ya kucheza na si kusugua benchi.

Tumeshuhudia kwa misimu kadhaa iliyopita, wachezaji wengi wakikimbilia kusajiliwa na klabu kubwa nchini za Simba, Yanga na Azam FC kutokana na maslahi makubwa wanayolipwa, lakini wakaenda kuishia kusugua benchi hadi msimu unamalizika na baadaye kutolewa kwa mkopo, jambo ambalo linaua vipaji vyao.

Hivyo, kwa kuwa soka ndiyo kazi yao, haina maana yoyote ya kukimbilia kusajiliwa na timu kubwa na kwenda kuishia benchi, lakini katika hilo pia kama wapo wachezaji ambao tayari wamejiunga na klabu hizo kubwa, wanapaswa kulewa sasa natakiwa kupambania namba na si kubweteka tu na mishahara pamoja na posho kubwa wanazolipwa huku vipaji vyao vikiteketea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Mwenye moyo wa kuonywa huonywa

**ANAYESIKILIZA** na kufuata mashauri anayopewa hufaidika. Methali hii hutumiwa kutufunza tuwe na tabia ya kuyasikiliza na kuyafanya mashauri tunayopewa na wanaotuzidi ujuzi au maarifa tusije fikwa na maafa au majuto baadaye.

Leo nimeamua kuwaonya mashabiki (watu wenye mapenzi na hamasa) wa Simba na Yanga wamesema maneno mabaya dhidi ya upande mwingine ilhali timu zao zipo eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam zikiwa timu za mwanzo kuanzishwa humu nchini.

Wahenga walitahadharisha kuwa "Mwenye moyo wa kuonywa huonywa." Maana yake anayesikia na kuyafuata mashauri anayopewa hufaidika. Twafunzwa tuwe na tabia ya kuyasikiliza na kuyafuata mashauri tunayopewa na wanaotuzidi ujuzi au maarifa tusijefikwa na maafa au majuto baadaye.

"Ni lipi lisilo nduguje na mwamu wake?" Yaani ni jambo au tukio lipi ambalo halina, linalohusiana nalo au jenzake (ndugu au mwamu?) Methali hii hutumiwa kumkumbusha mtu kwamba awafanyiapo wenzake mabaya lazima hata yeye ataishia kufanyiwa mabaya. Tuwafanyiayo wenzetu watatufanyia hayo nasi. Pia hutukumbusha kuwa kila jambo lina jingine linalohusiana nalo.

Kwa hali hiyo husemwa: "Nia njema tabibu, nia mbaya huaribu." Yaani lengo zuri au azimio zuri ni kama dawa ilhali baya ni uharibifu. Methali hii hutumika kuwakumbusha watu umuhimu wa kuwa na nia njema au kuazimia kutenda mambo mema ambayo huwafaidia watu.

Husemwa: "Painamapo ndio painukapo" maana yake panapoinama huweza kuinuka siku moja au baadaye. Methali hii yaweza kutumiwa kumfariji mtu aliyekumbwa na shida na kumhimiza asikate tamaa kwa kuwa huenda akaishia kufanikiwa. Shida na matatizo huwa sehemu ya maisha ya binadamu. Mashabiki wa Yanga na Simba mpo?

"Penye nia pana njia" kwa mujibu wa wahenga. Ikiwa mtu ana dhamira ya kulifanya jambo fulani hawezi kuikosa njia. Methali hii hutumika kutukumbusha kwamba tuwapo na nia ya kulifanya jambo fulani lazima tutafanikiwa.

Kwa mashabiki wa Simba nawaambia: "Ukidhani umesimama uangalie usianguke." Maana yake udhaniapo umesimama unapaswa kuangalia usianguke. Hii ni methali ya kutumiwa kwa mtu anayejitapa kutokana na hali nzuri aliyo nayo, mathalani ya kiuchumi. Apaswa kukumbuka kwamba hali hiyo yaweza kuwaondokea na kubaki kama mwanzoni.

Kwa mashabiki wa Yanga nao nawaambia: "Ukikosa shukuru, kupata kuna Mungu." Ukosapo kitu mshukuru Mungu tu kwani ndiye mwenye uwezo wa kutoa. Hii ni methali ya kutumia kuwasihi watu wasiwe na tabia ya kulalamikalalamika kwani Mungu ndiye mwenye uwezo wa kila kitu.

Narudi tena kwa mashabiki wa Simba: "Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi." Maana yake usijivune kwa kwenda mbele, unaweza kurudi nyuma wakati wowote. Methali hii hutumiwa kumkanya na kumshauri mtu aliyepata cheo au mali kisha akajawa na kiburi na kuanza kuwadharau watu wengine, bila kujua inawezekana akafilisika na kuishia kuwa mtu duni.

Sasa nipo kwa mashabiki wa Yanga: "Walio chini ya munga (aina ya mti) sasa wako madarini." Maana yake waliokuwa wakiishi au wakikaa chini ya mti wa munga sasa wanakaa majumbani. Ni methali inayofaa kutumiwa kutukumbusha kuwa maisha ya watu hubadilika sana. Waliokuwa na hali nzuri na ya kujivunia huenda ikawaondokea na waliokuwa wanyonge wakafanikiwa. Yanga kumbukeni mlivyowananga Simba miaka ya nyuma! Kutesa kwa zamu.

Kwa pamoja nawazungumzia mashabiki wa Simba na Yanga, ila msinirushie mawe kwani mashabiki hawana simile wala subira; "Ulimwengu ni dhaifu siuoneni sheshe." 'Sheshe' ni kivumishi chenye maana ya kizuri kama vile 'nguo sheshe' ni nguo nzuri maana yake dunia au ulimwengu ni kitu dhaifu tusivutwe na sura yake ya uzuri.

Methali hii hutumiwa kumtahadharisha mtu anayejisifu na kujigamba kutokana na uwezo au nguvu alizo nazo ajue kwamba, ulimwengu unaweza kumwangamiza.

Bado nipo na mashabiki wa Simba na Yanga nikiwakumbusha walivyosema wahenga kuwa: "Mchimba kisima huingia mwenyewe." Maana yake mtu anayemchimbia mwingine shimo kwa dhamira mbaya huishia kuingia yeye mwenyewe. Hii ni methali inayoweza kutumiwa kumshauri mtu anayekusudia kumfanyia ubaya mwenzake kuwa huenda ubaya huo ukamrudia yeye.

Kilichompata ngwena (mamba) na kiboko ni hicho." Hatari inayoweza kumfika mamba lazima itamfika kiboko, kwa sababu wanaishi katika mazingira mamoja.

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784334096*

HABARI KITAIFA

# CHAKUA yajitosa chanjo ya corona

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), kimewataka viongozi wake wa ngazi zote, wanachama na abiria kujitokeza kupata chanjo ya corona ili kujikinga na ugonjwa huo.

Msemaji wa ofisi ya Mwenyekiti wa CHAKUA Taifa, Solomon Nkiggi, alisema chama hicho kimetoa wito huo kwa lengo la kuokoa maisha ya wanachama wake na abiria kwa ujumla.

"CHAKUA inatetea abiria juu ya haki zao mbalimbali na sasa imejitosa kuwaelimisha juu ya kujikinga na ugonjwa huo kwa kuchukua tahadhari zote zinazoelekezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto lakini pia kuchanjwa," alisema Nkiggi.

Alisema suala la chanjo ni la muhimu na kwamba wakiwa wadau wa usafiri, wameona washiriki kukamilifu kuelimisha abiria na kuhimiza chanjo kwa viongozi, wanachama na wasafiri wa ndani na nje ya nchi.

"Mwenyekiti wa CHAKUA, Hassan Mchanjama, ametoa wito kwa viongozi wa chama ngazi zote, wanachama na abiria kujitokeza kupata chanjo ya corona ili kujikinga na ugonjwa huo," alisema.

Alisema usalama wa abiria unaanzia kwenye afya yake na pia kuepuka ajali za barabarani na kwamba chama hicho kinahimiza hayo yote ili kila abiria awe makini tangu mwanzo wa safari hadi mwisho.

Kuhusu utetezi wa haki za abiria, Nkiggi alisema chama hicho huwa kinawaelekeza kujua kuwa wanapaswa kulipwa fidia kwa aliyepata madhara katika ajali, kutotozwa nauli kubwa bali iliyoidhinishwa na mamlaka husika.

"Tumekuwa pia tukitetea abiria wasikubali kukatiwa tiketi wakati gari husika halipo, wakatiwe tiketi inayoonyesha nauli halali wanayolipa, kuandikwa majina yao, kuchagua mabasi analotaka," alisema.

Pia alisema chama hicho hushirikisha wasafirishaji na kuwaelekeza kuzingatia wajibu wao wawapo safarini ikiwamo kutoendesha mwendo usioruhusiwa, na kwamba abiria wana haki ya kutoa taarifa polisi.

sambamba na hilo, alisema chama huwawakilisha abiria katika vikao vya wadau vya kupanga nauli na vingine vinavyohusu maslahi yao na huwatetea ili wapate haki kwa kuwajulisha polisi, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA), hata kwenda mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria inapoonekana haki zao zimekiukwa. kwa washiriki wa mtandaoni kutoka nje ya nchi.

# Vifo wajawazito, watoto vyashtua madiwani

**Na Gurian Adolf,** NKASI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, limeshtushwa na ongezeko la vifo vya wajawazito na watoto na kutaka kujua sababu ya tatizo hilo.

Hatua hiyo inatokana na taarifa iliyowasilishwa na kuonyesha kuwa kati ya Januari na Agosti, mwaka huu, wajawazito 15 na watoto 50, wamepoteza maisha.

Akiwasilisha taarifa ya vifo hivyo katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika jana, Mratibu wa Afya ya Mama na Mtoto wilayani hapa, Josepha Joseph, alisema vifo hivyo vimetokana na sababu mbalimbali ikiwamo wajawazito kuchelewa kufika katika vituo vya kutolea huduma za uzazi salama.

Joseph alisema kuwa sababu nyingine ni kuvuja damu nyingi wakati wa kujifungua, kuchanika mfuko wa uzazi na kondo la nyuma, matumizi ya dawa za jadi kwa ajili ya kuongeza uchungu pamoja na kutohudhuria kliniki.

Mratibu huyo alisema vifo 11 vya wajawazito vilitokea katika vituo vya kutolea huduma za uzazi salama, huku wawili walifariki dunia ndani ya gari la wagonjwa wakiwa wanasafirishwa kutoka katika zahanati kupelekwa kwenye vituo vya afya vinavyotoa huduma za upasuaji.

Kuhusu watoto waliofariki muda mfupi baada ya kuzaliwa, alisema sababu ni wajawazito kuchelewa kufika hospitalini, hivyo kuchelewa kupata huduma.

Kutokana na hali hiyo, alisema halmashauri imeweka mikakati mbalimbali ya kukabiliana na vifo hivyo ikiwamo kupatikana kwa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mkakati mwingine ni kuwa na watoa huduma wenye ujuzi, kuimarisha huduma za rufani ikiwamo upatikaniaji wa gari la wagonjwa kwa wakati na elimu kwa jamii ya kuwawahisha wajawazito katika vituo vya kutolea huduma.

Katika kikao hicho, Diwani wa Kirando, Anastazia Kasago, aliishauri idara ya afya katika halmashauri kuwakumbusha wahudumu wa afya kutambua kuwa kazi ya kuwahudumia wajawazito ni yao, hivyo waifanye kwa moyo wa upendo.

Naye Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Khenan, aliishauri idara ya afya kufanya utafiti, ili ibaini ni kwa nini baadhi ya wajawazito wamekuwa wakigoma kwenda kujifungulia hospitalini na badala yake wamekuwa wakikimbilia kwa wakunga wa jadi.

Pia aliwasihi baadhi ya wahudumu wa afya hasa wanawake waache tabia ya kuwanyanyasa wajawazito pindi wanapokwenda kujifungua katika vituo vya huduma kwa kuwa vitendo hivyo vinachochea ongezeko la vifo vya wajawazito na watoto katika halmashauri hiyo.



Mratibu wa Mwitikio wa Viongozi wa Dini wa Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA), Jovin Riziki akizungumza wakati wa semina ya viongozi wa dini na watu wanaoishi na VVU wakijadilia kuhusu unyanyapaa na ubaguzi kama kikwazo kwa watu wanaoishi na VVU, iliyoandaliwa na Mtandao wa Kimataifa wa viongozi wa dini inayojisisha na watu wanaoishi na VVU (TANERELA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Marekebisho mawasiliano ya habari yaja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeleta rasimu ya marekebisho ya kanuni nne za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA).

Kuletwa kwa rasimu hiyo kunatarajiwa kusaidia kutenganisha watoa huduma za maudhui mtandaoni kama chombo cha habari na wale wanaotoa maudhui ambayo hayahusiani na chombo cha habari.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imewakutanisha wadau wa Sekta ya Mawasiliano na Habari Jijini hapa, kujadili na kutoa maoni kuhusu kanuni hizo ambazo ni kanuni za leseni, kanuni za maudhui mtandaoni, kanuni za miundombinu ya utangazaji kidijitali na kanuni za maudhui ya redio na runinga.

Wadau waliotoa maoni kuhusu rasimu hiyo ni pamoja na Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa (CORI), Baraza la Habari Tanzania (MCT), MISA Tanzania, Umoja wa Kampuni za Simu Tanzania (TAMNOA), Wamiliki wa Vyombo vya Habari (MOAT), wamiliki wa ving'amuzi na Jukwaa la Wahariri Tanzania.

Akizungumza juzi wakati wa ukusanyaji wa maoni, Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji wa TCRA, Dk. Philip Filikunjombe, alisema maboresho ambayo wadau wanatolea maoni yataleta mabadiliko katika sekta ya mawasiliano na habari.

Alisema maoni hayo yatasaidia kutenganisha kati ya watoa huduma za maudhui mtandaoni kama chombo cha habari na wale wanaotoa maudhui ambayo hayahusiani na vyombo vya habari.

Dk. Filikunjombe pia alisema maboresho hayo yatatatua sintofahamu ya nani anatakiwa kupatiwa leseni ya kuweka maudhui mtandaoni pamoja na kushusha ada ya leseni hizo.

Alisema maombi ya leseni kwenye rasimu hiyo imeshuka kutoka Sh.100, 000 hadi Sh. 50,000 na ada ya leseni kwa mwaka imeshuka kutoka Sh. milioni moja hadi Sh. 500,000 kwa mwaka.

Pia alisema kanuni zilizopo kwa sasa zinawataka watoa huduma wa redio na runinga kuomba leseni ya kutaka maudhui yaleyale kuonekana mtandaoni lakini kutokana na rasimu hiyo hawatatakiwa kuomba leseni tena ili vipindi vyao kuonekana kupitia mtandao.

Dk. Filikunjombe alisema maboresho ya kanuni hizo kuwa yanaenda kupunguza ada ya leseni ya kurusha matangazo ya redio na runinga kwa asilimia 30 na kuruhusu vituo vya redio na runinga kujiunga na vituo vingine kurusha maudhui yao bila kupata kibali kutoka TCRA.

Alisema watakachotakiwa kufanya ni kupeleka mpangilio wa vipindi unaoonyesha kuwa atajiunga na kituo kingine.

# Waziri ataka kutengwa maeneo ya uwekezaji

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amewataka wakuu wa mikoa na makatibu tawala nchini kutenga maeneo maalum, kwa ajili ya uwekezaji.

Alisema hayo jana katika ziara ya viongozi hao wa mikoa 26, wilayni hapa kwa ajili ya kujifunza namna wilaya hiyo, ilivyofanikiwa kutumia fedha za ndani katika miradi ya maendeleo na kutenga sehemu maalum kwa wawekezaji.

Wakuu hao wa mikoa, jana walitembelea eneo la uwekezaji wa viwanda vinane, lenye ukubwa wa ekari 600 na sehemu maalum, kwa ajili ya wajasiriamali yenye ukubwa wa ekari 500 wilayani hapa.

Waziri Ummy alisema Manispaa ya Kahama, ambayo imeongoza kwenye ukusanyaji mapato, ilipanga kukusanya Sh. bilioni 8.8, lakini ilivuka lengo kwa kukusanya Sh bilioni 9.6 sawa na asilimia 109.

Alisema manispaa hiyo ilipanga kupeleka Sh. bilioni 4.7 katika miradi ya maendeleo, lakini wamefanikiwa kupeleka Sh Bilioni 5.1

"Ni Manispaa ambayo imefanikiwa kuanzisha 'business park' kitu ambacho maeneo mengine wanatakiwa kujifunza na kwenda kuanzisha kwenye maeneo yao," alisema Waziri Ummy.

Aliwataka viongozi hao kutenga maeneo ya uwekezaji kama ilivyofanya Manispaa ya Kahama na kwamba yasiwe porini na ambayo hayapitiki.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, alisema mwekezaji mzawa, Mhoja Ndegesera, amewekeza Sh. bilioni 250 kwenye viwanda vinane na serikali ya mkoa itaendelea kumuunga mkono.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, alisema wametenga eneo la uwekezaji la Chapulwa lenye ukubwa wa ekari 600, kwa ajili ya viwanda na mwekezaji wa kampuni ya Kom Company Ltd, Ndegesera, alipatiwa ekari 90 bure na kwa mwaka mmoja wamerudisha Sh. milioni 140.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Judith Nguli (kulia), akikabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Hashim Komba, katika Kijiji cha Lionja, kwaajili ya kuanza kuukimbiza wilayani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wazazi wachangishana 500/- kuwalipa walimu

**Na Happy Severine,** BARIADI

WAZAZI wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kidinda iliyopo mjini hapa, wamekubaliana kuchanga Sh. 500 kila mwezi ili kuwalipa walimu wa sayansi ambao si waajiriwa wa serikali ili wafundishe watoto.

Uamuzi huo unatokana na uhaba walimu wa masomo ya sayansi shuleni hapo, hali ambayo husababisha wanafunzi kutofanya vizuri katika masomo hayo.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Shule hiyo, Mhinga Malongeta, wakati akipokea vifaa kwa ajili ya maabara ya teknolojia ya habari na mawasiliano vilivyotolewa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCAF).

Malongeta alisema shule hiyo inakabiliwa na uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi kwa kipindi kirefu na kusababisha wanafunzi kutofundishwa vipindi vilivyopangwa katika ratiba.

Alisema shule hiyo ina mwalimu mmoja wa masomo ya sayansi aliyeajiriwa na serikali na inakuwa vigumu kwake kufundisha wanafunzi wote wa madarasa ya sayansi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Kwa mujibu wa mkuu huyo, shule hiyo ina wanafunzi 1,075 na mwalimu wa masomo ya sayansi yupo mmoja kwa kila somo hali inayomfanya ashindwe kumudu kufundisha wanafunzi wote.

Alisema kutokana na hali hiyo uongozi wa shule kwa kushirikiana na wazazi walikubaliana kuajiri walimu wa muda kwa kuwalipa kiasi kidogo ili wanafunzi hao wasikose masomo.

# DC ahimiza ushirikishwaji wananchi kubuni, kuibua miradi ya maendeleo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, amewataka madiwani kuwashirikisha wananchi kuibua miradi kwenye maeneo yao badala ya kusubiri serikali kwenda kutekeleza miradi ambayo inawezekana si ya kipaumbele kwao.

Msafiri aliyasema hayo jana kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kibaha Mjini huku akisisitiza kwamba ushirikishwaji ni muhimu kwa jamii.

Alisema hakuna miradi ambayo serikali inaweza kutekeleza yenyewe bila kuibuliwa na wananchi.

"Madiwani kupitia vikao vya kata wawashirikishe wananchi kuibua miradi ya maendeleo ambayo itakuwa na faida kwao kuliko kuiachia serikali ambayo haitakuwa na majibu ya kipaumbele chao kwenye maeneo wanayoishi," alisema.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema kuna masoko yameanzishwa na wananchi na serikali inayaendeleza kwa kuboresha miundombinu ili huduma zitolewe kwenye mazingira mazuri. Pia aliwaelekeza wananchi kwenye maeneo yanayotoa huduma za kijamii kama shule na vituo vya afya ambayo vina upungufu na uchakavu waanze kujenga maboma na serikali itamalizia.

Msafiri alisema ziko baadhi ya shule miundombinu yake imechakaa, hivyo wananchi wanaposhirikishwa wanachangia nguvu kazi na serikali inamalizia walipoishia.

Naye Diwani wa Kongowe, Hamis Shomari, alisema vyumba vya madarasa kwenye shule zilizoko katika kata hiyo wananchi wamekuwa wakihamasishwa kuchangia nguvu kazi na serikali imekamilisha hali inayopunguza mlundikano wa wanafunzi katika chumba kimoja.

Shomari alisema maelekezo yaliyotolewa na mkuu wa wilaya yataendelea kufanyiwa kazi ili kuondoa vikwazo vya maendeleo katika maeneo yao

Katika kikao hicho wajumbe wa halmashauri kuu walifikia maazimio ya wataalamu wa afya kutoa elimu ya chanjo ya corona ili kuondoa baadhi ya mikanganyiko kwenye jamii ambayo inaleta hofu.

Wajumbe hao walisema wataendelea na uhamasishaji kwenye maeneo yao kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kupata chanjo ya corona.

Saimon Mbelwa, Mwenyekiti CCM Kata ya Kongowe, alisema wataalamu wanapaswa kufika kwa wananchi waelezee faida za kuchanja na kuwatoa hofu ili Rais aone mapokeo chanya kutoka kwa wananchi wakichanja kwa wingi.



# Bunge lataka watoto mitaani wakusanywe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imeiagiza serikali kuwakusanya watoto wa mitaani walioko katika maeneo mbalimbali nchini na kuwaweka katika vituo ili kuwapatia mahitaji yao ya msingi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, alitoa agizo hilo juzi wakati wa ziara ya kamati hiyo kutembelea na kukagua Makao ya Taifa ya Watoto yaliyoko Kikombo, nje kidogo ya Jiji la Dodoma.

Nyongo alisema tatizo la watoto wa mitaani nchini ni kubwa na wengi bado wanahitaji kupata huduma zinazotolewa na vituo vya kulelea watoto.

"Niendelee kuwasihi Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuendelea kuwaleta watoto wa mitaani katika vituo kama hivi ili waje wapate huduma zinazotolewa kwani tatizo hili bado kubwa sana huko mtaani," aliagiza.

Nyongo alisema kuwa kutokana na kituo hicho kuwa cha kipee, serikali inatakiwa kuweka nguvu kwenye maslahi ya watumishi wanaohudumia watoto.

"Kituo hiki ni cha kipekee, hivyo watumishi waliopo hapa mnatakiwa kuwaangalia sana hasa katika maslahi yao. Kama yatakuwa na wasiwasi basi hata watoto hawa watakuwa katika malezi yasiyofaa," alisema.

Pia alisema kutokana na kituo hicho kuwa na uwezo wa kuhudumia watoto zaidi ya 250, jitihada za kuwakusanya na kuwaleta watoto kutoka maeneo mbalimbali zinatakiwa kufanyika.

"Taarifa yenu inadai kuwa hadi sasa kuna watoto 54 lakini kituo hiki kinao uwezo wa kuhudumia watoto zaidi ya 250, hivyo kamati inaagiza kuleta wengine ikiwamo wale kutoka Kituo cha Kurasini, Dar es Saalam waje hapa na waondolewe kule ambako mazingira sio mazuri," aliagiza.

Mjumbe wa Kamati hiyo na Mbunge wa Viti Maalum (CHAD



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (kulia), akionyesha jengo la utawala katika Makao ya Taifa ya Kulelea Watoto Kikombo, kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, walipofanya ziara jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Stanslaus Nyongo. **PICHA: WAMJW**

# Shule 700 kunufaika mradi elimu ya awali

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

SHIRIKA linalojihusisha na masuala ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto la Children in Crossfire (CIC) limepanga kuzifikia shule za msingi 700, mkoani Dodoma, katika utekelezaji wa Mradi wa Watoto Wetu Tunu Yetu.

Mradi huo unalenga kuboresha elimu ya awali kwa kushirikiana na serikali na wadau katika mikoa husika.

Meneja wa Mradi huo kutoka CIC, Frank Samson, alisema hayo juzi jijini hapa alipozungumzia shughuli zinazofanywa na shirika hilo katika kikao kilichowakutanisha wadau wanaotoa huduma ya elimu msingi.

Kikao hicho kiliandaliwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Alisema shirika hilo linatekeleza mradi huo katika mikoa mitatu kwa kushirikiana na mashirika wenyeji, Mwanza (TAHEA), Morogoro (CDO) na Dodoma (Maarifa ni Ufunguo).

"Kwa Mkoa wa Dodoma ni Wilaya za Kongwa na Chamwino, tulianza mradi na shule za mfano 58 mwaka 2020 na kwa mwaka 2021, tumeweza kuzifikia shule zote 232 katika wilaya hizo," alisema.

Frank alisema kwa mwaka huu mradi huo umezifikia shule 92 katika Mikoa ya Morogoro na Mwanza, lakini lengo lao ni kuzifikia shule zote za mikoa hiyo.

Alisema shughuli zinazofanywa katika mradi huo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu wa elimu ya awali, kuboresha mazingira ya kujifunzia, kutoa mafunzo ya uongozi wa elimu kwa ngazi mbalimbali, kuboresha miundombinu kwa kujenga vyumba vya madarasa na vyoo.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita jumla ya vyumba 30 vya madarasa vimekamilika na vingine 50 viko kwenye mpango.

Frank alisema jumla ya vyumba 324 vya madarasa ya elimu ya awali vimekarabatiwa ndani ya mwaka 2020/21.

Alisema mradi umeshirikiana na jamii kuweka mifumo ya maji shuleni, ili kuhamasisha watoto kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.

Vilevile, alisema mradi huo umeimarisha ushirikiano wa shule na wazazi, ambao umechangia upatikanaji wa lishe kwa baadhi ya shule, ufuatiliaji wa ujifunzaji wa watoto shuleni na nyumbani, elimu ya jinsia pamoja na ulinzi wa mtoto.

"Mafunzo ya walimu wa awali yanalenga kupata walimu bora wa elimu ya awali, kuongeza umahiri wa ufundishaji, kutengeneza na kuendeleza mazingira ya kujifunza kwa kutumia vifaa vilivyopo kwenye mazingira, ili kuchochea utoaji wa elimu bora ya awali kwa watoto," alisema.

# Bil. 310/- kutumika Dodoma mwaka huu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKOA wa Dodoma umeidhinishiwa zaidi ya Sh. bilioni 314 katika mwaka wa fedha 2020/21 ambapo kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Januari, shughuli za serikali zimeendelea katika kila sekta kwa mafanikio makubwa.

Sekta hizo ni pamoja na ukusanyaji wa mapato ya serikali, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, sekta za kilimo na vyama vya ushirika, mifugo na uvuvi, elimu, afya, miundombinu, maji, ardhi na makazi na usambazaji wa umeme.

Akiwasilisha juzi jijini Dodoma taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema katika mwaka huu wa fedha, mkoa uliidhinishiwa zaidi ya Sh. bilioni 314.

Alisema kati ya fedha hizo, zaidi ya Sh. bilioni 109 zilikuwa ni fedha za maendeleo zikihusisha fedha za ndani zaidi ya Sh. bilioni 68 na fedha za nje zaidi ya Sh. bilioni 41.

Mtaka alisema katika kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu, mkoa ulipokea zaidi ya Sh. bilioni 109 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambapo kiasi hicho ni sawa na asilimia 35 ya bajeti na fedha ya miradi ya maendeleo zaidi ya Sh. bilioni 24.

Alisema fedha za mishahara ni zaidi ya Sh. bilioni 79 na za matumizi mengine ni zaidi ya Sh. bilioni tano, akifafanua kuwa fedha za maendeleo zinajumuisha za ndani Sh. bilioni 18 na za nje Sh. bilioni sita.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema makadirio ya makusanyo ya ndani kwa mwaka huu ni zaidi ya Sh. bilioni 61 na kwamba hadi Juni, mwaka huu, makusanyo yalikuwa ni zaidi ya Sh. bilioni 49, sawa na asilimia 81.22 ya lengo.

Mtaka alisema mkoa umeendelea kutenga fedha kutokana na mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo alidai halmashauri saba hupaswa kutenga asilimia 40 na Halmashauri ya Jiji la Dodoma inatakiwa kutenga asilimia 60 ya mapato yake ya ndani.

Alisema katika mwaka huu wa fedha, zaidi ya Sh. bilioni 27 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye halmashauri saba za Mkoa wa Dodoma.

"Kutokana na fedha zilizotengwa, mkoa umetekeleza miradi mingi katika sekta za afya na elimu," alisema.

Vilevile, alisema mkoa umeendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kutoa mafunzo pamoja na mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Alibainisha kuwa mwaka huu mkoa ulipanga kusajili vikundi 584 vya wajasiriamali wadogo na kuvipatia mafunzo ambapo vilivyosajiliwa ni 563 ikiwa ni sawa na asilimia 96 vikijumuisha vikundi 298 vya wanawake, 149 vya vijana na 51 vya watu wenye ulemavu.





# Makamu wa Rais aahidi mageuzi makazi, ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali imedhamiria kuleta mageuzi katika maendeleo ya makazi, biashara na uendelezaji ardhi ili kiwe kichocheo cha ukuaji wa uchumi Zanzibar.

Othman aliyasema hayo jana alipofungua kongamano na mkutano wa pili wa taasisi ya wataalamu wa milki kuu Tanzania huko katika Hoteli ya Verde iliyoko Mtoni, Zanzibar.

Alisema migogoro ya ardhi iliyopo bado ni tatizo kubwa linalohitaji juhudi za makusudi kupatiwa ufumbuzi wa haraka na kwamba wataalamu wanaweza kuwa na mchango mkubwa katika kupatikana suluhisho sahihi la tatizo hilo.

Alisema kongamano hilo linalowakutanisha wataalamu mbalimbali wa masuala ya ardhi, uwekezaji, wathamini wa majengo na maofisa ardhi, litasaidia kujadili na kutafuta njia mwafaka za matatizo ya ardhi ili kuifikisha Tanzania katika uchumi bora kupitia tasnia hiyo.

Makamu wa Rais alisema suluhisho la migogoro ya ardhi likipatikana, wananchi watatekeleza ipasavyo majukumu yao ya kilimo, ufugaji na ujenzi kwa tija zaidi kuliko ilivyo sasa.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mabadiliko katika sheria ya kukuza na kuendeleza uwekezaji Zanzibar, yakilenga kufungua fursa zaidi za uwekezaji kwa upande wa Kisiwa cha Pemba kwa nia ya kukuza uchumi na maendeleo ya Zanzibar.

Aliongeza kuwa mabadiliko hayo ya kisheria pia yamelenga kuongeza fursa na vivutio vipya vya uwekezaji wa biashara ya majengo pamoja na wanunuzi wa nyumba zilizoko katika miradi ya uwekezaji Unguja na Pemba.

Aliwakumbusha wataalamu wa mipango miji kuelewa kwamba nchi imevurugika kwenye eneo hilo na ipo mitaa mingi ambayo maeneo yake yengekuwa ya kuvutia na yenye haiba na thamani kubwa lakini kukosekana na kutosimamiwa mipango miji ipasavyo, kumefanya mitaa hiyo kuwa duni na isiyo na thamani.

'Ninaamini mipango miji na usimamizi wake ni moja ya mambo muhimu sana katika kubadili, sio tu haiba bali pia thamani ya ardhi na majengo.

"Mipango miji na usimamizi wenye ufanisi ungefanya mabaraza yetu ya miji kuwa na mapato ya kutosha kutekeleza kazi zao," alifafanua.

Rais wa Taasisi ya Wataalamu wa Milki Kuu Tanzania, Andru Katto, alisema Tanzania inashuhudia ongezeko kubwa la biashara ya majengo ambapo usimamizi wake husimamiwa na watu wasiokuwa wataalamu wa sekta hiyo.

Alisema jambo hilo ni kinyume kulinganishwa na nchi nyingi ambazo uuzwaji wa nyumba hufanywa na mawakala waliosomea na kujisajili chini ya sheria maalum zinazokuwapo.

Aliwataka wataalamu na washiriki wa kongamano hilo kushirikiana na serikali katika kuyatafutia ufumbuzi matatizo ya ardhi ikiwa ni pamoja usimamizi holela wa biashara ya majengo.



Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Udhibiti wa Nishati Afrika Mashariki, Dk. Geoffrey Mabea (kushoto), akimkabidhi Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, andiko la mradi kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Udhibiti wa Nishati Afrika Mashariki ambayo inatarajiwa kujengwa nchini Tanzania, alipofika ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar jana kujitambulisha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Samia kushiriki tamasha la Kizimkazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan, leo anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kilele cha tamasha la Kizimkazi (Kizimkazi Festival).

Kilele cha tamasha hilo lililoanza Agosti 23, kinatarajiwa kufanyika katika Uwanja wa Kizimkadi Dimbani ambako pia kutakuwa na uchomaji wa chanjo ya corona kwa mwananchi anayehitaji chanjo hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, aliwataka wananchi wa Mkoa wa Kusini Unguja na mikoa mingine kujitokeza kwa wingi katika tamasha hilo na kuchanja chanjo ya corona.

"Mimi na familia yangu yote kesho (leo) tutakuja kuchanja chanjo ya corona katika tamasha la Kizimkazi," alisema kiongozi huyo alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema katika tamasha hilo, Rais Samia atazindua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyojengwa na Benki ya CRDB kijijini huko ambapo ndipo kijiji anakotokea.

Katibu wa Kamati ya Kuratibu Tamasha hilo, Hamid Abdulhamid Khamis, alisema maandalizi yanaendelea vizuri ambapo sherehe hiyo inatarajiwa kuanza majira ya mchana.

Alisema katika kilele hicho, viongozi mbalimbali watahudhuria wakiwamo wageni kutoka nje ya nchi, viongozi wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mratibu huyo alisema tamasha hilo kwa kiasi kikubwa limedhaminiwa na CRDB na kumekuwa na utoaji wa zawadi kwa wanafunzi ikiwa ni sehemu ya shamrashamra ya tamasha hilo, ambapo wanafunzi bora katika shule tatu wamepatiwa zawadi kupitia benki hiyo.

"Tokea tulipoanza tamasha hili, viongozi mbalimbali walishiriki katika michezo tuliyokuwa nayo, ambapo tamasha lilifunguliwa na Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Maryam Mwinyi, mawaziri wa SMZ na Mkuu wa Mkoa na Wilaya yetu ya Kusini walishiriki kwa kiasi kikubwa sana, hivyo tunawashukuru sana kwa kutuunga mkono," alisifu.

Aliwataka wananchi kufika kwa wingi katika tamasha hilo na kwamba kutakuwa na burudani mbalimbali ikiwamo ngoma za asili.

# Wadhibiti wa nishati waiangukia serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wadhibiti wa Huduma ya Nishati ya Afrika Mashariki, wameiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuunga mkono jitihada za ujenzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Udhibti wa Nishati Afrika Mashariki ambayo inatarajiwa kujengwa nchini.

Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Wadhibiti wa Huduma za Nishati Afrika Mashariki, Dk. Geoffrey Mabea, alitoa rai hiyo alipozungumza na kujitambulisha kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ofisini kwake Vuga, Zanzibar.

Alisema jumuiya hiyo imepanga kujenga taasisi itakayotoa mafunzo kwa watu wake nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kitaalamu watendaji kutoka nchi wanachama.

Dk. Geoffrey alisema hatua hiyo itasaidia kuitangaza Tanzania na Afrika Mashariki kwa kuwaanda wataalamu wengi ambao watasaidia Afrikana dunia kwa ujumla katika masuala ya huduma za nishati.

Alisema jumuiya hiyo ambayo makao makuu yake yako jijini Arusha, tayari imekwishatayarisha masuala ya msingi kwa ajili ya utekelezaji wa azma hiyo ambapo viongozi wa jumuiya hiyo wanaendelea kutafuta eneo mahususi kwa ajili ya ujenzi wa taasisi hiyo ya mafunzo.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliwapongeza viongozi wa jumuiya hiyo kutokana na juhudi wanazozichukua katika kuimarisha udhibiti wa huduma za nishati kwa nchi za Afrika Mashariki na aliahidi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kutoa ushirikiano.

Hemed alisema ipo haja kwa jumuiya hiyo kuangalia namna bora ya utoaji wa huduma zinazoendana na mabadiliko ya teknolojia duniani ili kurahisisha zaidi gharama za uendeshaji wa huduma hizo.

Makamu wa Pili pia aliwaomba viongozi wenye dhamana ya usimamizi wa jumuiya hiyo kuangalia namna bora ya kuimarisha viwango vya nishati kwa kujifunza zaidi kutoka mataifa yalioendelea kwa lengo la kutumia mbinu mpya za kiuendeshaji.

Nchi zote ambazo ni wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kauli moja zimeshakubaliana taasisi hiyo ya mafunzo ya udhibiti wa nishati kujengwa nchini.



**DARASSA**
Uk.13



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



## NANCY SUMARI

# Tuipe muda Miss Tanzania itarudi imara kama zamani

MSHINDI wa Miss Tanzania mwaka 2006, Nancy Sumari, amezungumzia kudorora kwa shindano hilo akisema kunahitajika muda kurejea katika hali yake ya mwanzo kutokana na uongozi uliopo kuwa mpya.

Akiendelea na mahojiano na gazeti hili yaliyoanza kutolewa wiki iliyopita, Sumari amesema uongozi wa sasa unahitaji muda wa kuzoea na kubuni mbinu za kurudisha heshima kama ilivyokuwa zamani.

Amesema kuna nchi nyingine zina mikakati ya kitaifa kuhusiana na masuala ya urembo, hivyo kustawisha na kurudisha mapenzi ya wadau wote kukaa na kutafuta suluhisho.

Aidha, ameeleza hivi sasa soko la urembo limebadilika kutokana na watu kutumia mitandao ya kijamii kujinadi kama wanamitindo.

"Urembo sio kama vile wakati wetu, kwani sasa imebadilika sana unaweza kujisimamia mwenyewe kwa kuweka picha mtandaoni, imekuwa rahisi," amesema.

Mlimbwende huyo amesema ushindi wake wa Miss Tanzania, umesaidia kutoa maoni yake kila shindano hilo linapofanyika.

"Nina kawaida ya kuwaeleza wasichana wanaoshiriki pale ambapo nilianguka, ili wao waweze kutumia fursa katika kushinda," amesema Sumari.

### UREMBO UMEMPA HESHIMA

Hata hivyo, Sumari amesema anajivunia kushiriki Miss Tanzania, kwa sababu kama lisingekuwa shindano hilo asingepata heshima aliyonayo.

"Wakati mwingine watu wanauliza mbona mashindano ya urembo yameshuka, ni kwa vile yalikuwa yana umhimu, kwangu mimi naona yamenipa heshima na siwezi kusahau," ameongeza.

BASI SAWA

## Jose Chameleon azidi kuimarika



HALI ya mwanamuziki wa Uganda, Jose Chameleon, yaelezwa inazidi kuimarika baada ya kulazwa hospitalini tangu wiki iliyopita akiwa mahututi.
Chameleon ametoa ujumbe wake wa kwanza kwa mama yake mzazi, akimshukuru kwa kumpambania maisha yake na kumuonyesha upendo katika kipindi kigumu.
"Ahsante Mama, upendo wako uko dhahiri, hujawahi kukata tamaa juu ya ukweli, nitakua na nguvu ya kujifunza kutoka kwako. Mungu akujalie uzima zaidi" ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram.

## Ebitoke ameanza kutoka mate



MCHEKESHAJI maarufu, Ebitoke, amesema hakuna msanii mwenye maadili na kuulinda muziki wa Bongo Fleva kama Ali Kiba.
Kupitia page yake ya Instagram Ebitoke ameweka video ya Alikiba akiimba wimbo wake mpya wa 'Songi Songi' ambao ameurudia kutoka kwa msanii Maud Elka.
"King ni mmoja tu wa Bongofleva wengine endeleeni kuimba Amapiano zenu, huyu ndio mfalme anayetulindia Bongofleva yetu" ameandika.



## Manfongo huo sasa ushamba

BAADHI ya mashabiki wa muziki wamemponda mwanamuziki nyota wa singeli Manfongo, ambaye hivi karibuni alisema gari lake limemuongezea chuki kwa watu.

Mashabiki hao wamesema mwanamuziki huyo anaonekana kutoficha tabia yake halisi, kwani gari ni jambo la kawaida kwa sasa na hakuna mtu anayeweza kumjengea chuki kwa kuwa na chombo hicho.

Manfongo alikaririwa akisema mtu asiyemiliki gari anakuwa na makasiriko zaidi kuliko yule ambaye ana miliki gari yake.



## Akwegwe Mkwe: Mkwe kichefuchefu

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA ina maajabu sana. Kuna mambo yanaweza kutokea yakakushangaza na kujiuliza ni kwa nini yametokea. Lakini ndiyo dunia.

Baadhi ya mambo unaweza kuyaona kwenye filamu hii ya 'Akwege Mkwe'. Ni filamu inayomzungumzia, mama mmoja aliyesababisha kutokea mambo ya aibu kwa kijana wake kijiji anakoishi.

Halafu yeye anajiona kama yuko sawa, ila wenzake ndiyo wamekosea.

Imechezwa na Bi Zuki, Mariamo Bilal, Zuweta, Wakutengwa, Salulo Hamisi, Rajim Materu, Mariam Kidoti na na wengineo.

Bi Zuki ana kijana wake anaitwa Wakutengwa. Wakutengwa ana mke anaitwa Stamili. Historia inaonyesha kuwa mama huyo alimuokota Stamili akiwa na miaka miwili. Akamlea. Akakua. Akamuozesha kwa kijana wake Wakutengwa, ambaye mwanzo alidhania kuwa ni dada yake.

Bi Zuki ni mama mwenye tamaa. Wakati kijana wake akiwa safarini kikazi akawa anataka kumkuwadia mke wa mtoto wake wanaume na pesa achukue yeye. Binti anakataa. Ugomvi ukaanza.

Akaanza kumwambia kijana wake kuwa aachane na mwanamke huyo kwa sababu anapokwenda safari kikazi anaingiza mabwana. Kijana haamini.

Mama mkwe anafanya hila kwa kutia pilipili maji ambayo yaliandaliwa na Stamili ili mumewe akaoge.

Inamuingia machoni na kulia. Hiyo inampa fursa mama kumlazimisha kijana wake amfukuze. Anafanya hivyo.

Stamili hata ndugu. Anakokwenda hakujulikani. Anakutana na rafiki ya mumewe, Salulo ambaye anaamua kumpeleka kwake. Kesho yake anaenda kwa rafiki yake kumuombea msamama inashindikana.

Sakulo naye alikuwa ametengana na mkewe Zuweta. Wakati Sakulo anakaa na shemeji yake, Wakutengwa yeye ananzisha mahusiano na Zuweta mke wa rafiki yake. Mwisho wa siku kijiji kinakuja kubaini kuwa Zuweta ana ujauzito wa Wakutengwa na Stamili ana ujauzito wa Sakulo. Marafiki wamebadilishana wanawake. Kisa ni mama mkwe. Baadaye anakuja kuligundua hilo wanaombana msamaha. Kila mmoja anamchukua mkewe, akiwa na mimba na mwenzake. Hakuna aliyekuwa na kinyogo, kiroho safi, lakini wakimlaumu mama mkwe kichefuchefu aliyesababisha yote hayo.





## Darassa kufunga ndoa kimyakimya?

IMEELEZWA harusi kati ya rapa maarufu nchini, Darassa na mpenzi wake wa siku nyingi ipo mbioni na wakati wowote wawili hao watafunga ndoa.
Wiki iliyopita Darassa alimvisha pete ya uchumba mpenzi wake huyo, huku baadhi ya wasanii maarufu wakishuhudia tukio hilo.

Kulingana na watu wake wa karibu, Darassa anapanga kufanya harusi hiyo kuwa ya kifamilia zaidi na maandalizi yanafanyika kwa kasi.
"Wakati wowote tunaweza kumuona Darassa amefunga ndoa, maandalizi yanafanyika kwa familia zote mbili," kilisema chanzo hicho.

## Hidaya ya Pepe Kale hadi Leila

**Na Adam Fungamwango**

NYIMBO za zamani zilikuwa na mambo mengi sana ambayo wengi walikuwa hawajafahamu. Mara nyingi zilikuwa na historia ya kweli na watu walioimbwa walikuwa wapo vile vile. Wakati mwingine hata visa vilivyokuwa vikiimbwa vilikuwa vya kweli kabisa.

Mfano leo nitawaletea nyimbo za watu ambao wamesababisha kuwapo na familia moja hivi, pamoja na matukio kadhaa yaliyoikumba.

**Atikapo-Kalombo Mwanza**

Wimbo huu ulitungwa mwanzoni mwa miaka ya 1980. Mtunzi ni mwanamuziki George Lalombo Mwanza. Ni mwanamuziki Mkongomani aliyekuwa akifanya shughuli zake nchini Kenya.

Alianzisha makundi mbalimbali nchini Kenya kama Orchestra Bwambe Bwambe na baadaye Super Bwambe. Ni bendi iliyotunga na kuimba nyimbo nyingi, chini ya uongozi wake.

Mwanamuziki huyu alizaa mtoto na mwanamke mmoja wa Kitanzania aitwaye Hidaya Khamisi Mtumwa. Mtoto huyo alikuwa ni wa kike, akapewa jina la Leila.

**Bishada-Skassy Kasambula**

Akiwa Super Matimila, Skassy, mwimbaji na mtunzi mahiri, mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1980, alitunga wimbo uitwao 'Bishada'. Wimbo huu alimtungia mkewe ambaye alifanikiwa kupata naye mtoto wa kiume aitwaye Belly.

Kuna kipande kimoja cha wimbo huo kinaimbwa hivi "Tupendane kwa roho moja, nia yangu mama tuiachane, nisije nikanywa sumu, kipenda roho Bishada thamani. Nikitoka ofisini, unipokee kwa furaha, kioo cha nyumba yangu, mama Belly."

**Christina Moshi-Skassy Kasambula**

Ni wimbo uliopigwa na Orchestra Safari Sound (OSS), wakati huo ikiwa kwenye mtindo wa Ndekule.

Kasambula ni mwanamuziki wa Kikongomani ambaye alipitia nchini, kwenye miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990, alipohamishia makazi yake nchini Kenya. Mtoto wake Belly, baadaye alimuoa Leila. Ni yule binti wa mwanamuziki Kalombo Mwanza, aliyezaa na Hidaya. Hao wawili baadaye wakaenda kuweka makazi yao nchini Uingereza.


**Hidaya-Pepe Kalle**

Mwishoni mwa miaka ya 1980, Hidaya Mtumwa, mama yake Leila, baada ya Kalombo kufariki, alikutana na mwanamuziki mwingine wa Kikongomani, Kabasele Yampanya, maarufu kama Pepe Kalle, jijini Arusha, Empire Bakuba ilipozuru Tanzania kufanya maonyesho. Alipoondoka Pepe Kalle alimtungia wimbo maarufu ulioitwa 'Shikamoo Seye', maarufu kama Hidaya. Pepe Kalle alifariki mwaka 1998, na Hidaya alifariki Julai mwaka huu.

**Leila-Twanga Pepeta.**

Ilikuwa ni mwanzoni mwa miaka ya 2000, bendi ya African Stars ilipopiga nyimbo mbili 'Busu la Mwaka 2000' na 'Busu la kufungwa Mwaka.'. Leila aliyeimbwa kwenye nyimbo zote mbili ni binti wa Hidaya wa Pepe Kalle, aliyeolewa na Belly mtoto wa Skassy.

Kwa bahati mbaya sana Leila alifariki nchini Uingereza mwaka 2018, kwa kile kilichodaiwa kuwa aliuawa na mumewe.



# Kanye West abadili jina



RAPA maarufu Kanye West, amewapa wakati mgumu mashabiki wake baada ya kueleza kuwa yupo mbioni kubadili jina lake hilo kisheria.

Kanye West, hatajulikana kwa jina lake hilo, badala yake atafahamika kwa maneno ya herufi mbili pekee 'Ye'.

Mwanamuziki huyo amekuwa na tabia ya kuwatania mashabiki wake katika kuwatambulisha Albam yake mpya 'Donda' inayotarajiwa kutoka hivi karibuni.

Hata hivyo, sasa inaonekana kuacha mambo hayo huku akionekana kuweka nguvu katika utambulisho wa jina lake jipya, ambalo anataka kuitwa rasmi.



## Destiny mshukuru Mungu

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Destiny Etiko, amenusurika kifo katika ajali mbaya ya gari wakati akirudi katika mazishi ya rafiki yake Stanley Okoro.

Nyota huyo wa filamu, alikuwa katika gari hilo pamoja na rafiki yake mwingine Kevin Ovo, akiwa kama abiria ndipo gari hilo lilipata ajali na kumjeruhi.

Kulingana na taarifa zilizopatikana gari la wasanii hao liligongana uso kwa uso na basi lililokuwa linakwenda kwa kasi.

## Sadiya ukitoka huko utasimulia

MWIGIZAJI wa Nigeria, Sadiya Haruna, amehukumiwa kwenda katika mafunzo ya Sheria baada ya kupatikana na hatia ya kupotosha watu katika mitandao yake ya kijamii.

Hukumu hiyo imetolewa na mahakama moja ya Kiislamu katika jimbo la Kano, baada ya kuthibitisha amefanya kosa hilo na kumpatia nafasi ya kwenda kusoma Sheria katika kipindi hicho, ili aelewe vyema.

Amedaiwa kuwa mara kwa mara alichapisha video zisizo na adabu, za uongo na kutoa maoni yake ya kijinsia kwenye akaunti zake za mitandao.

Mwigizaji huyo alikiri mashtaka ya unyanyasaji na tendo lisilofaa, ambalo linapingana na kifungu cha 355 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu 2000.





## Mambo yameisha, sasa kazi tu

RAPA Khaligraph Jones kutoka Kenya na Blaq Bonez wa Nigeria, hatimaye wamefungua ukurasa mpya baada ya kuzika tofauti zao.

Ugomvi kati ya wasanii hao wawili ulianza mwaka jana baada ya Khaligraph kushinda tuzo ya MVP huko Nigeria.

Maadui hao wameonekana studio wakiwa pamoja wakihisiwa wako mbioni kupika ngoma yao mpya, huku Bien Sol wa Sauti Sol wakihusika kuwapatanisha.

## Maria, Nini wafanya umbea BBNaija

WIKI hii shindano la Big Brother Nigeria (BBNaija), limetawaliwa na mjadala mkali kuhusu washiriki wawili Maria na Nini, ambao walionekana kuwateta wapenzi wao waliowaacha nje ya nyumba hiyo.

Washiriki hao kila mmoja alisema jinsi wapenzi wao wanavyowaamini na endapo itatokea jambo lolote watavunjika moyo na inawezekana hawatasamehewa.

Maria kwa upande wake amesema mpenzi wake anaonekana kutokuwa na mapenzi ya dhati, lakini hapendi kumuudhi. Nini alimwambia yeye anamuamini sana mpenzi wake na japo wakati mwingine anakuwa kimya kwa kila kitu anachokifanya yeye.



# MIAKA 24 TAYOA

## ●Yafanikiwa mapambano dhidi ya UKIMWI
## ●Serikali yamwagia sifa kuwanusuru vijana

**Na Joseph Mwendapole**



Mkurugenzi Mkuu wa TAYOA, Peter Masika (kushoto) akizungumza jambo na Waziri wa Tamisemi, Ummy Mwalimu katika moja ya shughuli zilizofanywa na shirika lake. **PICHA: MTANDAO**

SHIRIKA la Vijana la Tanzania (TAYOA), limekuwa kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa miaka 24, likiwa limepata mafanikio makubwa kwa kuelimisha vijana na watu wa rika mbalimbali kujitambua na kuchukua hatua za namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU.

Miaka mingi ya safari ya mapambano dhidi ya UKIMWI, tena bila kupoteza mwelekeo, imelifanya shirika hilo kupongezwa na serikali kwa jitihada zake zilizoonekana waziwazi.

Kipindi chote shirika hilo limekuwa likibuni mbinu kadha wa kadha za kuwafikia watu wa rika mbalimbali, kuanzia njia ya simu za bure, kuwatembelea waliko na kuwahamasisha kuchukua hatua za kujilinda.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Peter Masika, amekuwa mfano wa kuigwa kwa ubunifu ambao amekuwa akionyesha ili kuwafikia vijana kwa urahisi na kuwapa elimu ya UKIMWI.

Mara kadhaa amekuwa akiwashauri vijana kuachana na masuala ya ngono kabla ya muda ama wakishindwa kabisa watumie mipira kujilinda.

Wakati wa uzinduzi wa makasha ya kondom hivi karibuni mkoani Dodoma , Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alipongeza na kuelezea umahiri wa shirika hili katika kupambana na janga la UKIMWI kwa miaka yote tangu kuanzishwa kwake mwaka 1997.

Ummy anasema kwa miaka yote tangu kuanzishwa kwake shirika hilo limejikita kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI bila kupoteza mwelekeo kama wengine hivyo kuchangia kikamilifu jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

"Kwa miaka yote ambayo nimelijua shirika hili na kuwa nalo karibu limekuwa mstari wa mbele kupambana na UKIMWI, na kwa miaka yote hiyo hawajawahi kupoteza mwelekeo, kazi yao imekuwa moja tu, kupambana kuzuia maambulizi mapya ya VVU kwa vijana na watu wa rika zote na wamekuwa msaada mkubwa," alisema

"Na miaka hii wote macho yetu tumeelekezea kwenye mapambano dhidi ya COVID 19 lakini wenzetu TAYOA wameendelea kupambana na janga la UKIMWI wanatukumbusha kwamba wakati mnapambana na ugonjwa huo na UKIMWI bado upo hongereni sana kwa msimamo wenu," anaongeza Ummy.

Anasema shirika hilo mbali na kupambana na janga la UKIMWI imekuwa mstari wa mbele kutoa elimu sahihi kuhusu afya ya uzazi kwa kuwazuia vijana kuingia kwenye ngono wakiwa na umri mdogo hali ambayo mbali ya kuwahatarisha kupata VVU pia kupata ujauzito wa mapema.

"Pater amesema hapa kwamba hata wazazi tukisema kwamba hawafanyi tunajidanganya kwasababu wanafanya kwa hiyo njia bora ni kuwaelimisha namna ya kuepuka kupata VVU na mimba za utotoni, tusipofanya hivyo sisi kwa watoto wetu basi tutambue kuwa watafundishwa na mitandao," anasisitiza

Waziri Ummy, anaeleza kwamba jamii inapaswa kuachana na dhana kwamba wasichana na wanawake wanapokwenda kununua kondom huonekana kama malaya hali ambayo imewafanya kuwa waoga kununua kwaajili ya kujikinga.

Aidha, amepongeza ubunifu wa TAYOA wa kutengeneza ATM za kondom, kwani utaondoa hali hiyo na sasa wanawake na wasichana wataweza kununua zana hizo kwa usiri na kwenda kuzitumia kujilinda na magonjwa na mimba zisizo tarajiwa.

"Ningependa kuona ATM hizi na makasha ya kondom yanasambaa nchi nzima kwenye halmashauri zote 184 ili mtu ajihudumie mwenyewe kwa usiri nawaomba watumishi kwenye halmashauri zote TAYOA watakapokuja muwape ushirikiano wafanye kazi zao vizuri," Waziri Ummy anazidi kusema.

Mkurugenzi wa TAYOA, Peter Masika, anasema tangu taasisi hiyo ilipoanzishwa mwaka 1997 imekuwa ikiwahamasisha watu wajilinde dhidi ya umaskini, ujinga na maradhi na limefanikiwa kuwafikia mamilioni ya Watanzania hasa vijana ambapo mbali na elimu ya Ukimwi wanapewa elimu ya ujasiriamali.

"Mwaka 2023 TAYOA tunaadhimisha Jubelei ya miaka 25 ya kuwatumikia Watanzania hasa vijana, imeanzisha familia ya kampuni ya kijamii ya Vijanatz Industries ambayo itatumia mbinu za kibiashara kutatua changamoto za vijana katika safari yao ya maisha," anasema

Anasema kwa kutambua ukubwa wake na kwa uzoefu wake katika kazi za vijana kwa kushirikiana na vijana asasi hiyo imekuwa ikifikiria sana juu ya safari ya maisha ya vijana.

TAYOA ina historia ya kutoa mafunzo ya mabadiliko ya tabia pamoja na zana zake (kondom) katika kutekeleza mbinu za kupambana na maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini.

Masika anasema hali hiyo ndiyo iliwafanya wajikite katika kuangalia kwa undani tatizo la maambukizi mapya ya VVU kwa vijana ambapo wasichana wanaongoza kwa asilimia kubwa pamoja na juhudi zote za kuelimisha wakagundua kuwa waanakosa zana za kujilinda.

"Hivyo kwa kushirikiana na vijana wenyewe tukabuni aina hizi za makasha ya kusambaza kondom za bure na kusaidia kupeleka kondom karibu na watumiaji wanapohitaji. Pia tukaona ni bora kuingiza kondom zenye ubora zilizotengenezwa kwa teknolojia ya kisasa kabisa na kuziuza kwa bei nafuu kupitia kampuni ya Vijanatz Industries," anaeleza

Masika anasema kwa sasa Tayoa inashirikiana na AMREF kutekeleza mradi wa GLOBAL FUND unaowalenga wasichana waliokatika umri balehe na wanawake vijana katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Tanga, Singida na Geita.

Alisema kundi hilo liko katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU magonjwa ya ngono na mimba zisizotarajiwa na kwamba TAYOA imekuwa ikishirikiana na kampuni zote zinazotoa huduma za mawasiliano Tanzania kutoa huduma za ushauri nasaha na mabadiliko ya tabia kupitia huduma za simu bila malipo kwa namba 117 vijanahelpline.

Masika anasema tayari zaidi ya vijana milioni tano wameshafikiwa na washauri wa TAYOA akiongeza kuwa pamoja na kundi hilo kuwa katika hatari zaidi ndilo kundi ambalo linapata changamoto nyingi kweli katika kupata na kutumia kondom.

"Hata kwenye jamii yetu tunamoishi mwanamke akiwa na kondom anaonekana Malaya wakati hali haiku hivyo kwa wanaume jamii lazima itambue kuwa mwanamke naye anahaki ya kujilinda," alisema Peter Masika

# BONDE LA PANJSHIR

## Eneo dogo linaloogopwa nchini Afghanistan

## Taliban wahofia kulitwaa, wengi wameangamia



Bonde la Panjshir

**Na Mwandishi Wetu**

PAMOJA na kundi la Taliban kudhibiti nchi yote ya Afghanistan, lakini kuna eneo moja dogo hawajaweza kuligusa na itawachukua muda mrefu kulitwaa kwenye mikono yao.

Eneo la bonde la Panjshir, limekuwa la kushangaza kutokana na ugumu wake wa kuingia na kulitawala kiasi ambacho majeshi ya Urusi na Marekani iliwachukua miaka kadhaa kulidhibiti.

Kila kundi lililofanikiwa kuweka ngome yake katika bonde hilo, ilikuwa vigumu kuwakabili kutokana na eneo hilo kuwa na vizuizi vya milima na kuwa kielelezo cha misukosuko ya kihistoria nchini Afghanistan.

Kutokana na unyeti wake, miaka ya 1980 likuwa ngome muhimu kwa vikosi vya jeshi la Wasoviet na kuanzia 1990 walikuwa Taliban.

Hata hivyo, kwa sasa eneo hilo linadhibitiwa na kundi National Resistance Front of Afghanistan (NRF), ambalo linahasimiana na Taliban.

"Jeshi la serikali na washirika wake walishindwa kulidhibiti na Taliban kwa miaka 25 iliyopita, walijaribu kulichukua lakini walishindwa, walikutana na kipigo kibaya," anasema Ali Nazary, kiongozi wa NRF wa masuala ya mahusiano ya kimataifa wakati akizungumza na BBC.

Bonde hilo lenye kina kirefu na lenye kutawaliwa na vumbi la udongo, liko maili 75 kama kilometa 120, kusini magharibi mwa mji mkuu wa Afghanistan, Kabul.

Bonde hilo linazungukwa na milima mirefu yenye urefu wa mpaka futi 9,800 kama kilometa 3 kutoka usawa wa bonde lenyewe.

Milima hii inatumika kama vikwazo vinavyowasaidia watu wanaoishi hapo wasiweze kufikiwa kirahisi.

Kuna barabara nyembamba ya kuingia kwenye eneo la bonde hilo ambayo hupita katikati ya miamba mikubwa ya mawe na mto Panjshir.

"Hili sio bonde moja, ukiingia ndani utakutana na mabonde madogo karibu 21 yaliyounganika," anasema Shakib Sharifi, aliyewahi kuishi hapo wakati wa utoto wake, lakini aliondoka Afghanistan baada ya Taliban kushika hatamu.

"Kihistoria bonde hili la Panjshir linafahamika pia kwa uchimbaji wa madini," anasema Elisabeth Leake, profesa kutoka chuo kikuu cha Leeds, Uingereza.

Maelfu ya wanapiganaji wanaolipinga kundi la Taliban nchini Afghanistan, wanaripotiwa kukabiliana na kundi hilo wakiwa wamejificha kwenye bonde lililo ndani, lenye njia jembamba la kuingilia kama maili 30 kutoka mji mkuu, Kabul.

Bonde hili lina mabwawa yanayofua umeme. Marekani ilisaidia ujenzi wa barabara za eneo hilo na kuweka mkongo wa radio ambao unapokea mawasiliano kutoka Kabul.

Kambi ya wanajeshi wa anga wa Marekani, ambayo awali ilijengwa na Warusi miaka ya 1950, pia iko karibu tu na mlango wa bonde hilo.

'Watu wenye akili'

Inakadiriwa kati ya watu 150,000 na 200,000 wanaishi katika bonde hilo. Wengi wakizungumza lugha ya kabila la Dari , moja ya lugha kuu nchini humo.

Kabila hilo ni kama robo moja ya watu wote milioni 38 wa nchi hiyo ,lakini watu wanaoishi kwenye bonde Panjshir wana utambulisho wao.

Sharifi ambaye alikuwa mkurugenzi mkuu wa mipango kwenye wizara ya kilimo ya Afghanistan, anasema watu wa eneo hilo wana akili sana.

Anasema watu hao hawapatani na Taliban na wanasifa ya ugomvi, lakini ugomvi wao ni wa namna nzuri. Ushindi wa kihistoria dhidi ya Waingereza, Warusi na Taliban, ulizidi kuwatia moyo zaidi watu wa eneo hilo.

Baada ya Taliban kushindwa na kuondolewa madarakani mwaka 2001, bonde hilo likapandishwa hadhi kutoka wilaya na kuwa jimbo. Moja ya majimbo madogo nchini Afghanistan.

Hata hivyo uamuzi wa kuipandisha hadhi na kuwa jimbo ulikuwa wenye utata.

Inafahamika wapiganaji wa Panjshiri walikuwa na nguvu sana katika miaka ya 2000, walisaidia kuirejesha serikali na kuwa mshirika namba moja.

Katika kuwapa asante, viongozi wa Panjshiri walipewa nafasi maarufu kwenye serikali na jeshi.

Bonde hilo likawa huru na likawa bonde pekee nchini Afghanistan liliiloogozwa na magavana wenye asili ya hapo, na sio kutoka nje ya eneo hilo.

"Kawaida gavana anatakiwa kuwa mtiifu kwa serikali kuliko watu anaowaongoza, kwa Punshir, ilikuwa tofauti," anasema Dkt. Giustozzi.

**BONDE LA MIKAKATI**

Kulingana na Dk. Giustozzi, kuna uwezekano kuwa yapo mabonde mengi yanayofanana na hilo nchini Afghanistan. Lakini ukaribu na barabara kuu kaskazini mwa Kabul unaipa umuhimu mkubwa wa kuwa la kimkakati.

Sharifi anasema umuhimu wa bonde la Panjshir ni muunganiko wa sababu nyingi.

"Maofisa wa serikali ya Afghan wenye mahusiano na Panjshir walipeleka silaha nyingi kwenye bonde hilo kwa sababu walikuwa na hofu kuhusu marais Karzai na Ghani, lakini mwishowe ni Taliban ndio waliokuwa na hofu zaidi." Anaongeza kusema.

Hata hivyo, mtu anayeongoza wapiganaji wa Panjshir wanaopingana na Taliban ni kijana wa miaka 32 pekee ambaye anaitwa Ahmad Massoud.

Massoud ni mtoto wa aliyekuwa kiongozi hapo kati ya miaka ya 1980 na 90 Ahmad Shah Massoud.

Baba yake aliyejulikana kwa jina la utani kama "Simba wa Panjshir", alikuwa kamanda wa Mujahidina aliyeongoza kuwafurushwa Warusi na Taliban waliotaka kuvamia bonde hilo.

Massoud aliwahi kusema kwamba wapiganaji wake wanapata msaada wa kijeshi kutoka kwa baadhi ya maofisa wa jeshi la Afghanistan na jeshi maalumu la taifa hilo.

**BONDE LILILOSHINDIKANA**

Kati ya mwaka 1980 na 1985, warusi walianzisha mashambulizi ya ardhi na anga. Wapiganaji wa Urusi waliokuwa na uzoefu mdogo na eneo hilo, walishambuliwa vibaya.

Maelfu ya wanajeshi wa Kirusi walijeruhiwa kutoka kila upande wa milima.

Dk. Giustozzi anasema vikosi vya urusi vilifanikiwa kuliteka bonde hilo, lakini kwa muda mfupi.

"Warusi hawakuona maana ya kukaa pale na kuwaweka wanajeshi wake pale ilikuwa changamoto kubwa," anasema.

"Walitaka kulinda barabara kuu ya kaskazini kusini, lakini mapigano yalizuka katika maeneo mengine ya karibu." Anaongeza kusema.

Unapofika eneo hilo utaziona silaha, vifaru na ndege ziliachwa na wanajeshi zikiota kutu kama kumbukumbu ya kushindwa wanajeshi wa Urusi.

Dk. Giustozzi anasema katika kipindi hicho, Massoud alikuwa tofauti na viongozi wengine wa waasi.

"Alikuwa msomi, anayeweza kuzungumza kifaransa, anaongea taratibu na alikuwa mcheshi.

Hata hivyo Mzee Massoud aliuawa mwaka 2001 na kundi la al-Qaeda, siku mbili kabla ya mashambulizi ya Septemba 11, 2001, yaliyofanywa na kundi hilo.

**NINI KITATOKEA?**

Ahmad Massoud aliyekuwa na miaka 12, wakati baba yake anafariki amechukua uongozi akiwa msomi aliyesoma Uingereza.

"Ana haiba ya baba yake, lakini hajapata majaribu ya kuongoza vita," anasema Dk. Giustozzi.

"Pia anahitaji ujuzi wa kufanya mazungumzo na kujadiliana kuhusu mgawanyo wa madaraka kitaifa. Kwa sababu hiyo ni mgeni na hana cha kupoteza." Prof Leake anasema

Aidha anaongeza "Lakini kwa sasa mambo ni tofauti. Talibani wamechukua udhibiti wa karibu majiji yote makubwa na miji iliyo karibu na bonde hilo,hivyo uingizwaji wa bidhaa na silaha umekuwa mkubwa. Hili linaleta utofauti."

Massoud mwenyewe ameshaomba msaada kama wababe wa vita wa Taliban, ni wazi wataanzisha mashambulizi.

**BBC**



Mabaki ya helkopta ya Urusi, iliyotumika wakati wa uvamizi wa nchini Afghanistan mwaka 1979 katika bonde la Panjshir

# Rais Hichilema 'amtwisha'mzigo wa uchumi waziri mpya wa fedha

**Lusaka,** ZAMBIA

RAIS Hakainde Hichilema amemteua Situmbeko Musokotwan kuwa Waziri mpya wa fedha Zambia, huku akiwa na jukumu la kuimarisha uchumi nchini humo.

Jina la Musokotwan limetajwa jana. Waziri huyo ni mbobezi katika masuala ya uchumi kimataifa ambaye aliwahi kushika wadhifa wa naibu gavana wa Benki Kuu.

Musokotwan aliwahi kushika wadhifa wa uwaziri huo mwaka 2008 hadi 2011.

Rais Hichilema alichaguliwa kuwa rais mwanzoni mwa mwezi huu baada ya kumshinda mpinzani wake aliyekuwa rais wa taifa hilo Edgar Lungu, kwa mamilioni ya kura.

Rais huyo amehaidi raia wa Zambia kuboresha uchumi ambao ulikuwa umeshuka.

Hichilema alisema katika hotuba yake ya kuapishwa kwamba serikali yake itahakikisha kuwa raia wa nchi hiyo wanapata milo mitatu kwa siku.

"Hakuna Mzambia anayepaswa kwenda kitandani akiwa na njaa," Hichilema aliwaambia raia wa nchi hiyo waliokuwa wamefurika uwanjani katika mji mkuu, Lusaka.

Pia alisema serikali yake italenga kufufua uchumi na kubuni ajira kwa vijana wasio na ajira.

Rais Hichilema alimshinda kiongozi aliyekuwa mamlakani, Lungu kwa ushiindi wa kishindo siku 12 zilizopita.

Ilikuwa ni mara ya sita kwa mfanyabiashara huyo wa zamani kugombea urais.

Ushindi wa Hichilema mwenye umri wa miaka 59 umeleta matumaini kwa viongozi wenzake wa upinzani katika mataifa mengine ya Afrika kwamba wao pia wanaweza kushinda ukandamizaji wa taifa na siku moja wanaweza kupanda na kuwa mamlakani.

Katika hotuba yake Hichilema amemshukuru mtangulizi wake kwa kuwezesha kuwapo kwa makabidhiano rahisi ya mamlaka, aliongeza kuwa haikuwa kuhamisha mamlaka bali ilikuwa ni kuhamisha uongozi.

Aliongeza kuwa nchi inakabiliwa na changamoto nyingi lakini serikali itafufua uchumi, ambao amesema umekuwa ukizidiwa na ulipaji wa madeni, kulipa fidia na matumizi na hivyo kusababisha kuwapo kwa fursa ndogo ya uwekezaji kwa ajili ya ukuaji.

BBC




Waafghanistan wakipakia jeneza la mwenzao nje ya hospitali, aliyefariki kwa shambulizi la bomu kwenye uwanja wa ndege Kabul, Afghanistan, jana. Watu wawili walijitoa mhanga na kushambulia umati wa watu eneo hilo na kuua takribani watu 100 wakiwamo wanajeshi wa Marekani 13, juzi. **PICHA: AP**

# Mamia ya wanafunzi waliotekwa waachiwa huru Nigeria kwa fidia

**Lagos,** NIGERIA

MAKUMI ya wanafunzi kutoka chuo cha Kiislamu Magharibi mwa Nigeria, waliotekwa nyara karibu miezi mitatu iliyopita na sita kati yao waliofariki dunia wakiwa mikononi mwa watekaji nyara, wameachiliwa, mkuu wa shule hiyo ametangaza.

Mei 30, karibu watu 200 wenye silaha za kivita walivamia mji wa Tegina, Jimbo la Nigeria, Magharibi mwa Nigeria na kuwateka nyara wanafunzi 136 kutoka shule ya kibinafsi ya Waislamu Salihu Tanko.

Desemba, Nigeria imekumbwa na mfululizo wa visa vya utekaji nyara katika shule na vyuo vikuu.

Wanafunzi sita wa Tegina walifariki wakiwa mikononi mwa watekaji nyara na wengine kumi na tano waliweza kutoroka, Juni, mwaka huu kwa mujibu wa uongozi wa shule.

"Wanafunzi wote wameachiliwa. Tunawapeleka nyumbani," mkuu wa shule ya Salihu Tanko, Abubakar Alhassan ameliambia shirika la habari la AFP.

"Siwezi kutoa idadi kamili kwa sasa. Itabidi tuwaangalie mara tu tutakapofika nyumbani. Lakini hakuna mwanafunzi yeyote aliye mikononi mwa watekaji nyara."

Hakutoa maelezo kuhusiana na kuachiliwa kwa wanafunzi hao au kusema ikiwa walilipa fidia kabla ya kuachiliwa.

Maeneo ya Kaskazini Magharibi na katikati mwa Nigeria yanakabiliwa na ongezeko la mashambulio, uporaji na utekaji nyara, vitendo vinavyoendeshwa na magenge ya wahalifu wanaojulikana kijijini kama majambazi.

Mwaka huu, magenge hayo yalianza kulenga wanafunzi kwa kutarajia fidia.

RFI

# Biden kulipiza kisasi vifo Wamarekani 13 Afghanistan

**Kabul,** AFGHANISTAN

RAIS wa Marekani Joe Biden, ametoa onyo kali kwa magaidi waliohusika na mashambulizi karibu na uwanja wa ndege wa Kabul na kuahidi kulipiza kisasi akisema kwamba atawawinda popote walipo na kuwaadhibu.

Akizunguza katika hotuba aliyoitoa akiwa White House majira ya jioni, juzi, Biden alisema kundi la Islamic State tawi la Afghanistan liitwalo ISIS K ndilo lilihusika na mashambulizi ambayo yaliuwa wanajeshi 13 wa Marekani na dazeni za raia wa Afghanistan.

Biden aliyasema hayo huku ikithibitishwa kwamba pamoja na raia hao wa Marekani, zaidi ya Waafghanitan 60 walipoteza maisha yao kwenye mashambulizi hayo.

"Hatutawasamehe na hatutasahau," Biden alisema wakati wa hotuba yake kabla ya kujibu maswali kutoka kwa waandishi wa habari.

Alisema hakuna ushahidi kwamba washambuliaji walikula njama na Taliban ambao wanaidhibiti nchi.

Karibu Wamarekani 1,000 na Waafghanistan wengi wameshindwa namna ya kuondoka mjini Kabul. Zaidi ya watu 100,000 wamekwisha ondolewa Afghanistan kufikia sasa.

Mapema Alhamisi, milipuko miwili karibu na uwanja wa ndege wa Kabul, iliwaua wanajeshi wa Marekani na Waafghanistan waliokuwa wamekusanyika eneo hilo, wakijaribu kuondoka Afghanistan.

Kamanda wa Wanajeshi wa Marekani Afghanistan Jenerali Frank McKenzie, alisema katika mkutano wa waandishi wa habari kwamba, wanafuatilia matukio mjini Kabul kwa karibu.

Kundi la kigaidi la Islamic State limedai kuhusika na shambulio hilo.

McKenzie alisema, wataendelea kutekeleza jukumu yao makuu, ambayo ni kuwandoa Wamarekani na raia wengine nchini Afghanistan.

Alisema ISIS haitawazuia kufanikisha kazi yao.

Akizungumzia kuhusu milipuko wa kwanza, Ofisa wa Taliban ameiambia Sauti ya Amerika kwamba, mshambuliaji wa kujitoa muhanga amejilipua katika eneo kulikokuwa kumekusanyika watu wengi, wakiwemo wanawake.

Milipuko hiyo ilitokea saa kadhaa baada ya serikali za Magharibi kutoa onyo juu ya tishio la shambulio la kigaidi kwenye uwanja wa ndege na kuwaomba watu waliokuwa wamekusanyika eneo hilo wakisubiri kuondolewa Afghanistan, kujieleleza kwenye eneo salama.

Kufuatia milipuko hiyo, ubalozi wa Marekani mjini Kabul, umewataka raia wa Marekani kutoenda kwenye uwanja wa ndege na kuepuka milango ya uwanja huo.

VOA

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## PATA MKOPO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL).

KWA MAWASILIANO ZAIDI

TUPIGIE: 0677 111 333

AU 0758 112 332

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KAWE**
**(S.S. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo KAWE**
**Usimamizi wa mirathi 212 ya 2021**

Ombi la **CAROLINA NAIMAN PALANJO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **EMMANUEL ELIRINGIA MACHANGE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 23/9/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
**EMMANUEL ELIRINGIA MACHANGE**
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe
Mahakama ya mwanzo

Kinondoni, Kimara, Sinza, Ilala, Temeke, Mbagala, Ukonga, Kigamboni, Buguruni

116427302

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**MARK BASIL SALLA** anatangaza kupotelewa na kadi za gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye namba za usajili **T 272 CLN** chasis namba **RZN1470005702** engine namba **IRZ1637371** na kadi yangari ya **TOYOTA HARRIER** yenye namba za usajili **T 260 DKJ** chasis namba **SXU100032815** engine namba **5S1017337**,yeyote atakayeziokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KW/IR/3292/2020**

1164274 02

## ANATAFUTWA



Hemed Salum (Msimamizi wa mirathi ya marehemu Salum Seif Lwambo), anamtafuta Mohamed Selemani , kuweka sahihi nyalaka za kiwanja no 129, kitalu 2 Mwananyamala Dar es salaam

**Taarifa ya polisi OB/RB/7637/2021**

1164275 02

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALI MLEKWA ALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA CRESTA** yenye namba za usajili **T 291 AWB.**Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **MBZ/R-B/1073/2021.**

1164278 02

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.79 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE LEVINUS LEONARD MAPENZI**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARIA MASUMBUKO**
**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before 10 **Day of 09 /2021**

**Dated at Dodoma this 10TH day of August 2021**

**RESIDENT MAGISTRATE**

1164279 02

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SUSANA ADAM JOSEPH** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki **SINORAY** yenye namba za usajili **MC 764 CBH** chasis namba **LZSHCMZW1J8004794** engine namba **163FMLP8J700069,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa MUH/RB/2120/2021**

1164280 02

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **KELVIN STANLAUS MOSHI** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya pikipiki aliyo uziwa na kampuni ya **GS GROUP LIMITED** yenye usajili Namba. **MC 522 CNY Chasis Namba.LC6PC-JK21L0009395 Engine Namba.156FM15AD2F74907** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Rb Namba. **MOR/MOR/RB/419403/2021.**

1164281 02

## ANAMTAFUTA NDUGU YAKE



MIMI ENGINEER WILFRED D. DUNGAMU NAMTAFUTA NDUGU YANGU MWENYE PICHA HAPO JUU ANAYEJULIKANA KWA MAJINA RAYMUND CHINYAMA ALIYEKUWA AKIISHI TEGETA JIJINI DAR ES SALAAM,TUMEPOTEZANA TANGIA MWAKA 2007,

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**
**0754 368274**
**AU 0658 368274**

1164286 02

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**MUHIDINI MOHAMEDI MPINGA** anatangaza kupotelewa na kadi za gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T 370 DFK** na kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA/CERES** yenye namba za usajili **T 903 BCF,** yeyote atakayeziokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/419918/2021**

1164285 02

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**REHEMA SALUM NGWALE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T990 DDK** Lenye chases namba **RZH 1830003169** injini namba **2RZ3042564** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi **RB. Namba IRI/IRI/RB/420424/2021**


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Tedi bado alikuwa kwenye mshangao. "Hivi wewe Tom una wazimu? Yaani unaniruhusu nikatembee na Sam. Tena mtu ambaye anatembea na mkeo? Kwa hiyo atuchanganye wote wawili uone raha ee. Hivi wewe ni mwanaume gani? Mwanaume wa wapi?" Tedi aliongea kwa ukali na hapo akanyanyuka ili avae nguo zake.

Tom alimkamata kwa nguvu. Alimrudisha tena kitandani. Alijua maneno aliyosema ni kama kumdhalilisha. Kumtuma aende kwa mwanaume mwingine ni kumfanya kama ni mwanamke asiye na thamani.

"Tulia Tedi. Naomba tuelewane. Maana yangu siyo hivyo unavyodhani. Usidhani mimi ni mjinga kiasi hicho. Nitachotaka hapa ni msaada tu kwako kwa sababu tayari huyo Sam alikuwa na nia ya wewe. Nachotaka ni kwenda naye. Yeye akiwa na hamu na wewe, lakini unakwenda kwenye kazi maalum. Utakwenda huko nikiwa nimechukua hatua zote zitakazofanya asifanye chochote na wewe. Utakuwa ukifanya kila kitu kwa maelekezo yangu na kama ukiyafuata, hatokufanya chochote. Hatokugusa na wewe utapata ulichokifuata." Tom aliongea kwa msisitizo. Ni sauti ya mamlaka ambayo Tedi hakuwahi kuisikia kabla. Ilimfanya atue tuli.

"Siwezi kukupeleka kwa mwanaume mwingine. Kuanzia leo utakuwa chini yangu hadi hapo nitakapoupata ukweli wote kuhusu mke wangu Farida."

Ni maneno yaliyomshusha presha Tedi "Sawa, ila mi nitaweza kweli mimi. Naweza kuzuia kunifanyia unyama wowote, lakini kumlaghai na hayo maswali hadi tukapata ukweli, nitaweza?"

"Utaweza. Hakuna ninachoshindikana chini ya jua. Ili mradi tu ufuate maelekezo yangu. Nitakupa nyenzo zote na mbinu zote za kufanya, utaweza tu."

"Nikiweza utanipa nini?"

"Nitakupa zawadi nzuri sana ambayo hujawahi kupata kabla."

"Ipi?"

"Na sitokuacha."

Jibu hilo lilimfanya Tedi kuangua kicheko kikali cha kike.

"Unataka kunifanya mke wa pili ee..."

"Juhudi yako tu mama, unaweza ukawa mke wa kwanza."

Sasa vicheko vilikuwa pande zote




**"Ya nini niwahi kutembea wakati nilikuwa nabebwa na mama. Nilikuwa naweza kutembea, lakini sikutaka kwa sababu nilijua nikitembea tu, sitabebwa tena, nikajifanya siwezi, hadi miaka miwili, nimegoma tu." Wakati akiongea hayo, Tedi alikuwa kakauka kwa kucheka.**

mbili.

"Wewe kumbe una vituko ee, sasa umeshaoa, halafu mimi niwe mke wa kwanza tena."

"Si kuna watu wanapanda vyeo. Unaweza ukawa mmoja wao." Alijibu Tom huku wakiendelea kucheka, wakakumbatiana kwa furaha kila mmoja akina na hamu na mwenzake.

Ulikuwa ni usiku murua. Usiku uliosahaulika kwa wote wawili. Walikuwa kama wanasafiri kwenye nchi fulani wasioijua jina na kuvinjari huko kwa raha zao.

Walikuwa kama wanapaa angani, chini kukiwa na bahari, lakini miili yao haianguki chini.

Ghafla usingizi mzito uliwajia.

Ni Tedi ndiyo aliyemuamsha mwenzake. "Inuka upate supu." Alimuamsha kwa upendo na madaha.

"Tom alifumbua macho. Uchovu bado ulimkabili. Lakini mikono laini ya mwanamama Tedi ilimfariji.

"Yaani umeamka, mapema hadi umekwenda kununua supu?"

"Unashangaa hilo. Kwani kati ya mume na mke, nani huwa anaamka alfajiri kufanya usafi, au kumtayarishia mume maji ya kuoga na kifungua kinywa ili aende kazini?"

"Eeeh, basi mama umeshinda." Alijibu huku akikaa vizuri kwenye kiti.

"Wewe umekunywa?"

"Mimi nimekunywa chai, na chapati mbili."

"Kwa nini hujakunywa supu?"

"Leo tu sikuwa na hamu nayo."

"Ila mimi ndiyo ukaona nina hamu nayo?"

"He he, we mwanaume hujui kupendwa. Yaani nimekuletea supu, bado unalalamika tu. Au una wasiwasi nimekuwekea limbwata?"

"Kwa wewe kama ni limbwata weka tu, kama umeweka kidogo, basi chukua bakuli ukaongeze tena." Alisema na kusababisha Tedi kutikisa kichwa, kabla ya kuangua kicheko.

"Inavyoonekana wewe ulichelewa kutembea. Na mama yako angepata shida sana asingekuzaa."

"Ya nini niwahi kutembea wakati nilikuwa nabebwa na mama. Nilikuwa naweza kutembea, lakini sikutaka kwa sababu nilijua nikitembea tu, sitabebwa tena, nikajifanya siwezi, hadi miaka miwili, nimegoma tu." Wakati akiongea hayo, Tedi alikuwa kakauka kwa kucheka.

Mwenzake, muda huo alikuwa akikata vipande vya nyama na kuviteketeza tumboni.

"Ni hivi. Jioni twende kwenye baa ya Mwenda. Sam atakuja na mke wangu, au vyovyote vile. Akija heba fanya uchokozi wowote kwake. Uchokozi wa kike sina haja ya kukuambia. Mvutie ili akufuate. Halafu mpe ahadi. Lakini mwambie isiwe kwenye nyumba za kulala wageni. Iwe nyumbani kwake. Ninachotaka huko ni wewe kutafuta ushahidi ambao unaweza kutufanya, au kunifanya nijue kwa nini mke wangu Farida amefanya kitendo kile."

"Mhh, kazi ngumu, lakini mimi nitatafutaje ushahidi wakati tuko wote ndani. Na ataniachia vipi hivi hivi nitoke bila ya kunigusa?"

Aliingiza mfukoni na kutoa vidonge vinne vya rangi ya kahawia.

"Si anakunywa yule? Mtilie kidonge kimoja kwenye kinywaji chake. Mlazimishe anywe au mnyweshe kimahaba. Atazimika. Yaani atazirahi. Hatokufa. Ila akijitahidi sana atazinduka baada ya masaa 12." Alisema, lakini akiona kabisa sura kwenye hofu usoni mwa Tedi.

"We siyo askari kweli. Mbona mipango yako kama askari, maana naona unajua mengi. Halafu akizinduka si atajua kuwa ni mimi?"

"Wakati akijua hilo, sisi huenda tuko kilometa nyingi kutoka Morogoro."

Maneno hayo yalionekana kumpa kidogo nguvu Tedi. Picha ilimjia kuwa akifanikiwa kutekeleza mpango huo mgumu, Tom atamchukua na kwenda naye Dar es Salaam. Alianza kupata matumaini ya kuwa pamoja na Tom kwa muda mrefu. Alianza kupata faraja kuwa ataachana na kazi aiyoipenda ya ubaamedi ambayo unaifanya kwa asjili ya shida tu. Hata hivyo kilichomsumbua ni kutoingia kwenye moyo ya Tom.

Alikuwa hajaelewa kuwa ni kweli Tom ataondoka naye, au anamtumia, lakini akimaliza atatoroka, na huenda akamdhuru Sam na kumrudia mkewe Farida. Pamoja na yote aliamua kujaribu bahati yake.

"Kama ikishindikana akinitoroka na mimi nitatoroka na kurudi kwetu Manyoni." Alijiambia.

"Kumbuka, ukimuwekea hiyo dawa, usichukue kila kitu. Tafuta vitu ambavyo vinaweza kunisaidia mimi kupata ninachokihitaji. Na hiyo itakuwa ndiyo salama ya kutokukugusa. Nadhani nimeshakwambia kila kitu. Kilakinachonihusu na mke wangu unakijua. Tena nimekumbuka, hata simu yake chukua, halafu tutajua baadaye."

"He baba, sawa, ila umenipa mzigo mzito, maana mimi umenifanya sasa kama polisi mpelelezi."

"Ndiyo utaanza karatibu kujifunza."

"Enhee, kitu gani cha kwanza kinatakiwa?"

"Twende mjini kwanza. Nikakununie nguo nzuri za gharama. Halafu tupitia saluni, usuke mtindo ambao wewe ukisuka unakupendeza sana. Yaani leo jioni uwe kama malaika. Akikuona atababaika. Ila la muhimu. Akisema twende nyumba ya wageni, kataa kwa sabbu huko hatutopata kitu tunachohitaji, hata kama utamuwekea dawa."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

MECHI KALI
HOME
AWAY
MANCHESTER CITY
1.31 | 5.50 | 9.16
ARSENAL

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 450




# KIVUMBI LIGI YA MABINGWA ULAYA

**MANCHESTER, England**

BINGWA wa Ligi Kuu England, Manchester City, amepangwa kundi moja na Paris St-Germain, RB Leipzig na Club Bruges katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye Kundi A.

Mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Chelsea watakutana na wakali wa Serie A, Juventus, Zenit St Petersburg ya Urusi na Malmo kutoka Sweden kwenye Kundi H.

Manchester United wao, wamepangwa kuvaana na Villarreal, ambao ni mabingwa wa Ligi ya Europa waliowafunga kwenye fainali ya msimu uliopita, pia wapo Atalanta ya Italia na Young Boys ya Uswisi katika Kundi F.

Liverpool kwa upande wao wako kwenye Kundi B, ambalo linaonekana kama la kifo likiwa na timu za Atletico Madrid, Porto na AC Milan.

Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu itapigwa katika Uwanja wa St Petersburg huko Urusi Jumamosi ya Mei 28, 2022.

**Droo kamili ya Makundi:**

**Kundi A:** Manchester City, Paris St-Germain, RB Leipzig, Club Bruges
**Kundi B:** Atletico Madrid, Liverpool, Porto, AC Milan
**Kundi C:** Sporting Lisbon, Borussia Dortmund, Ajax, Besiktas
**Kundi D:** Inter Milan, Real Madrid, Shakhtar Donetsk, Sheriff Tiraspol
**Kundi E:** Bayern Munich, Barcelona, Benfica, Dynamo Kyiv
**Kundi F:** Villarreal, Manchester United, Atalanta, Young Boys
**Kundi G:** Lille, Sevilla, FC Salzburg, Wolfsburg
**Kundi H:** Chelsea, Juventus, Zenit St Petersburg, Malmo

# *Ronaldo, Juventus wajadili kuachana*

**TURIN, Italia**

TAARIFA kutoka katika vyanzo vilivyothibitishwa, mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo ameomba kuachana na klabu hiyo huku akitaka kuuzwa katika majira haya ya joto.

Juventus wanasubiri ofa rasmi kutoka katika klabu ya Manchester City, huku ikitarajiwa kufika saa chache zijazo na wataafikia makubaliano haraka iwezekanavyo.

Taarifa pia zinaeleza, wakala wa Ronaldo, Jorge Mendes anafanya kazi moja kwa moja na bodi ya Man City kukamilisha makubaliano ya sheria na mkataba binafsi wa Ronaldo.

Man City pia inataka kuuza baadhi ya wachezaji, ili kupata ada ya kumsajili Ronaldo na Juventus wanataka euro milioni 28 hadi 30.

Raheem Sterling anaweza kuondoka Man City ikiwa dau wanalolitaka likifikiwa.

Mshambuliaji, Gabriel Jesus atabaki Man City kutokana na kocha Pep Guardiola anataka kusalia na mshambuliaji huyo katika msimu huu wa joto.



## HABARI MICHEZO


,150,500

# JACKPOT

## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/08/21 | 17:00 | Brighton vs Everton | 2.31 | 3.27 | 3.16 |
| 02. 28/08/21 | 17:00 | Newcastle vs Southampton | 2.60 | 3.40 | 2.65 |
| 03. 28/08/21 | 17:00 | Huddersfield vs Reading | 2.42 | 3.20 | 2.86 |
| 04. 28/08/21 | 17:00 | Preston vs Swansea | 2.46 | 3.26 | 2.77 |
| 05. 28/08/21 | 17:00 | Luton Town vs Sheffield Utd | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 06. 28/08/21 | 18:00 | Celta Vigo vs Athletic Bilbao | 2.42 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 28/08/21 | 19:30 | Liverpool vs Chelsea | 2.45 | 3.36 | 2.86 |
| 08. 28/08/21 | 20:30 | Real Oviedo vs Tenerife | 2.60 | 2.85 | 2.95 |
| 09. 29/08/21 | 16:00 | Burnley vs Leeds | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 10. 29/08/21 | 16:00 | Angers vs Rennes | 2.85 | 3.20 | 2.50 |
| 11. 29/08/21 | 16:30 | Union Berlin vs Monchengladbach | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 12. 29/08/21 | 20:30 | Cadiz CF vs Osasuna | 3.01 | 3.01 | 2.56 |
| 13. 29/08/21 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Granada | 2.61 | 3.22 | 2.77 |


## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**JUMAMOSI - 28 - AGOSTI 2021**

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1665 | Derby vs Nottingham | 2.47 | 2.96 | 3.01 |
| 14:30 | 2028 | Cardiff vs Bristol City | 1.95 | 3.30 | 3.85 |
| 14:30 | 4399 | Manchester City vs Arsenal | 1.31 | 5.50 | 9.16 |
| 16:30 | 1504 | Arminia Bielefeld vs Eintracht Frankfurt | 3.33 | 3.53 | 2.08 |
| 16:30 | 2067 | Augsburg vs Bayer Leverkusen | 4.57 | 3.83 | 1.71 |
| 16:30 | 2223 | Mainz vs Greuther Furth | 1.67 | 3.97 | 4.67 |
| 16:30 | 2713 | Stuttgart vs SC Freiburg | 2.18 | 3.43 | 3.18 |
| 16:30 | 3292 | FC Koln vs VfL Bochum | 1.84 | 3.72 | 3.97 |
| 17:00 | 1079 | Fulham vs Stoke City | 1.83 | 3.31 | 4.44 |
| 17:00 | 1430 | Hull City vs Bournemouth | 3.30 | 3.30 | 2.13 |
| 17:00 | 1620 | Middlesbrough vs Blackburn | 2.15 | 3.16 | 3.41 |
| 17:00 | 2059 | Barnsley vs Birmingham | 2.22 | 3.11 | 3.30 |
| 17:00 | 2363 | Dundee Utd vs Hearts | 3.36 | 3.31 | 2.10 |
| 17:00 | 2668 | QPR vs Coventry | 2.22 | 3.25 | 3.16 |
| 17:00 | 2732 | Preston vs Swansea | 2.29 | 3.16 | 3.11 |
| 17:00 | 2834 | Newcastle vs Southampton | 2.49 | 3.42 | 2.77 |
| 17:00 | 3275 | West Ham vs Crystal Palace | 1.58 | 4.02 | 5.82 |
| 17:00 | 3427 | Luton Town vs Sheffield Utd | 2.78 | 3.13 | 2.53 |
| 17:00 | 3778 | Brighton vs Everton | 2.37 | 3.21 | 3.11 |
| 17:00 | 5053 | Norwich City vs Leicester | 4.11 | 3.66 | 1.86 |
| 17:00 | 5808 | Millwall vs Blackpool | 1.82 | 3.39 | 4.33 |
| 17:00 | 5897 | Huddersfield vs Reading | 2.30 | 3.20 | 3.06 |
| 17:00 | 5987 | Aston Villa vs Brentford | 2.00 | 3.47 | 3.73 |
| 17:30 | 4938 | FC Vizela vs Boavista | 2.75 | 3.20 | 2.51 |
| 18:00 | 3264 | Nice vs Bordeaux | 1.62 | 3.94 | 5.19 |
| 18:00 | 5656 | Celta Vigo vs Athletic Bilbao | 2.43 | 3.16 | 3.06 |
| 19:00 | 2435 | St. Gallen vs FC Zurich | 1.99 | 3.75 | 3.26 |
| 19:15 | 3360 | Basaksehir vs Kayserispor | 1.79 | 3.51 | 4.34 |
| 19:15 | 5483 | Yeni Malatyaspor vs Gaziantep BB | 2.31 | 3.56 | 2.77 |
| 19:30 | 2530 | Lazio vs Spezia | 1.36 | 5.23 | 7.85 |
| 19:30 | 4026 | Eupen vs RFC Seraing | 1.66 | 3.95 | 4.55 |
| 19:30 | 5354 | Bayern Munchen vs Hertha BSC | 1.16 | 7.76 | 12.94 |
| 19:30 | 5441 | Liverpool vs Chelsea | 2.47 | 3.26 | 2.91 |
| 19:30 | 5704 | Atalanta vs Bologna | 1.36 | 5.45 | 7.27 |
| 19:45 | 4717 | Cambuur vs Twente | 2.51 | 3.40 | 2.61 |
| 20:30 | 2594 | Elche vs Sevilla FC | 5.05 | 3.48 | 1.76 |
| 20:30 | 3113 | Real Sociedad vs Levante | 1.57 | 4.13 | 5.65 |
| 21:00 | 1012 | GO Ahead Eagles vs Sparta Rotterdam | 3.10 | 3.29 | 2.23 |
| 21:00 | 1719 | PSV Eindhoven vs Groningen | 1.35 | 4.95 | 7.72 |
| 21:30 | 1974 | FC Sion vs FC Lugano | 3.16 | 3.26 | 2.21 |
| 21:45 | 2294 | Besiktas vs Fatih Karagumruk | 1.55 | 4.23 | 5.12 |
| 21:45 | 3039 | Juventus vs Empoli | 1.33 | 5.34 | 8.46 |
| 21:45 | 3384 | Fiorentina vs Torino | 2.22 | 3.41 | 3.21 |
| 21:45 | 3799 | Union Saint Gilloise vs Standard Liege | 1.81 | 3.50 | 4.24 |
| 21:45 | 5042 | Hatayspor vs Alanyaspor | 2.25 | 3.41 | 2.96 |
| 22:00 | 1637 | Marseille vs St Etienne | 1.72 | 3.78 | 4.57 |
| 22:00 | 3868 | Willem II Tilburg vs PEC Zwolle | 2.13 | 3.30 | 3.30 |
| 22:00 | 5946 | Peterborough vs West Bromwich | 4.83 | 3.65 | 1.68 |
| 22:30 | 2866 | Famalicao vs Sporting Lisbon | 6.50 | 4.43 | 1.44 |
| 23:00 | 1201 | Betis vs Real Madrid | 3.95 | 3.75 | 1.87 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# GUARDIOLA AITAMANI MIKOBA TIMU YA TAIFA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ametangaza nia yake ya kuondoka Manchester City na kutafuta fursa katika kiwango cha kimataifa pindi mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Guardiola sasa yuko katika mwaka wake wa mwisho wa makubaliano yake, pale kwenye Uwanja wa Etihad, ambapo amekuwa akisimamia tangu Julai 2016.

Baada ya kuchukua nafasi ya Manuel Pellegrini, bosi huyo wa zamani wa Barcelona ameshinda mataji matatu ya Ligi Kuu England, makombe manne ya EFL na Kombe la FA wakati wa enzi yake na City.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 50, amesema hana mpango wa kuongeza muda wa kukaa na klabu hiyo, na kwamba analenga fursa na timu ya taifa.

"Baada ya miaka saba katika timu hii, nadhani itabidi nisimame," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nitalazimika kupumzika, angalia kile tumefanya, inavutia.

"Na katika mchakato huu, ningependa kufundisha timu ya taifa, Amerika Kusini au Ulaya, nataka kuwa na uzoefu huo."

# *Deschamps apuuzia usajili wa Mbappe*



**PARIS, Ufaransa**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps amesema sakata la usajili wa Kylian Mbappe "sio dili" wakati 'Les Bleus' hao wakijiandaa kwenye mechi za kufuzu michuano ya Kombe la Dunia.

Mbappe anataka kuondoka Paris Saint-Germain na Real Madrid wameripotiwa kujaribu kufikia makubaliano na miamba hao wa Ligue 1.

Licha ya kwamba Mbappe, mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, Madrid wanaaminika wametoa ofa ya euro milioni 180, kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Wakati mabingwa hao wa dunia wakijiandaa kwenye mechi za kufuzu dhidi ya Bosnia-Herzegovina, (Septemba 1), Ukraine (Septemba 4) na Finland (Septemba 7) kuelekezea Qatar 2022, Deschamps aliulizwa kuhusu Madrid wanavyomtaka Mbappe.

"Siwezi kumjibia (Kylian Mbappe)," alisema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari. "Ni bora ukamuuliza yeye Swali hilo kuhusu majaliwa yake.

"Jambo pekee la msingi ni kwamba, soko la usajili linafungwa

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# JORGINHO, NYOTA CHELSEA WATAWALA TUZO ZA UEFA

●●● Kocha Tuchel naye abeba yake, huku Haaland akichomoza kuwa mshambuliaji bora kwa...

**NYON, UFARANSA**

NYOTA Jorginho ametwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa kiume wa Shirikisho la Soka Ulaya (Uefa), baada ya kuisaidia Chelsea kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Italia kwenye mashindano ya Euro 2020.

Kocha wake, Thomas Tuchel, ameshinda tuzo ya kocha bora wa mwaka, huku Edouard Mendy akitwaa tuzo ya golikipa bora na N'golo Kante kiungo bora.

Tuzo ya mshambuliaji bora imekwenda kwa Erling Haaland wa Dortmund na Norway, huku beki bora akichukua Ruben Dias wa Manchester City.

Kwa upande wa wanawake, Alexia Putellas wa Barcelona na Hispania ametwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka, huku Lluis Cortes wa Barcelona akitwaa tuzo ya kocha bora.

Tuzo ya kipa bora ya wanawake imechukuliwa na Sandra Panos wa Barcelona na Hispania, huku nafasi ya mlinzi bora imekwenda kwa Irene Paredes wa Barcelona na Hispania.

Kiungo bora wanawake imechukuliwa na Alexia Putellas wa Barcelona na Hispania na mshambuliaji bora ikienda kwa Jennifer Hermoso wa Barcelona na Hispania.

## ZISIKUPITE

### RONALDO SAFI MAN CITY

MANCHESTER City na Juventus zimekubaliana kuhusu uhamisho wa mshambuliaji Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36. ***(AS)***

### JESUS ATAKIWA JUVENTUS

JUVENTUS bado wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala wa Cristiano Ronaldo. ***(Sky Sports)***

### AUBAMEYANG HAONDOKI ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ametupilia mbali uwezekano wa nahodha na mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang kuondoka klabuni hapo. ***(ESPN)***

### SPURS YAKWAMA KWA TRAORE

KLABU ya Wolverhampton Wanderers imekataa ofa ya mkopo kwa ajili ya winga wake raia wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 25 kutoka Tottenham Hotspur, wakitaka kumbakiza. ***(Telegraph)***

### WEST HAM YAMTAKA VLASIC

WEST Ham United inamnyemelea mshambuliaji wa CSKA Moscow na Croatia, Nikola Vlasic, mwenye umri wa miaka 23, wakiendelea kutafuta mbadala wa kiungo mshambuliaji wa Manchester United na England, Jesse Lingard. ***(Sky Sports)***

### SISSOKO AWINDWA WATFORD

KLABU ya Watford imeanza mazungumzo na Tottenham Hotspur kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa Ufaransa, Moussa Sissoko mwenye umri wa miaka 32. ***(Fabrizio Romano)***

### PSG BADO YAMTAKA POGBA

KLABU ya Paris St-Germain inaendelea kusaka wachezaji akiwamo kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka, 28, na mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa 21, wakati huu wakijiandaa kumkosa Kylian Mbappe. ***(L'Equipe, via Mail)***

### MADRID HAIPOI KWA MBAPPE

REAL Madrid imeongeza dau lake kufikia pauni milioni 145 kwa ajili ya mshambuliaji wa Ufaransa na PSG, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 22, baada ya dau lake la awali la pauni milioni 137 kukataliwa. ***(Sky Sports)***

### MADUEKE AONGEZA MKATABA

MANCHESTER United imemkosa winga wa timu ya Taifa ya England chini ya miaka 21, Noni Madueke mwenye umri wa miaka 19, baada ya nyota huyo kusaini mkataba mpya na klabu yake ya PSV Eindhoven. ***(Mirror)***

### KANE MSHAHARA JUU SPURS

NAHODHA wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, yuko kwenye mazungumzo kuhusu kuboresha mkataba wake. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anatarajia kulipwa mshahara utakaofikia pauni 400,000 kwa wiki. ***(Times)***

### KOUNDE AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA inakaribia kumsajili mlinzi wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, katika uhamisho utakaogharimu pauni milioni 42. ***(Sky Italia, via Star)***

# HABARI MICHEZO

## Chirwa, Makame watua Namungo

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wawili wa zamani wa klabu ya Yanga, Obrey Chirwa na Abdulaziz Makame, wamejiunga na Namungo FC kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na michuano mingine.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Omary Kaaya, alisema wachezaji hao wamejiunga na Namungo baada ya kumaliza mikataba kwenye klabu walizotoka.

"Ni kweli tumewasajili wachezaji hao kama mlivyoona kwenye mitandao ya kijamii, na tumewasajili baada ya kumaliza mikataba kwenye klabu zao. Hivi ninavyoongea wapo mazoezini kwenye kambi ya msimu mpya wa ligi," alisema Kaaya.

Straika huyo, Chirwa, ambaye pia ana uwezo wa kucheza kama winga, amejiunga na klabu hiyo akitokea Azam FC, timu ambayo alijiunga nayo mwaka 2018, akitokea klabu ya Nagoon FC ya Misri baada ya kuachana na Yanga aliyoichezea kuanzia mwaka 2016, akitokea FC Platinum ya Zimbabwe.

Kwa upande wa Makame, amejiunga na Namungo FC akitokea klabu ya Polisi Tanzania ambayo alikuwa akichezea kwa mkopo kutoka Yanga.

## Ruvu Shooting sasa kujichimbia Mbweni

**Na Donald Lukele, TUDARCo**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, amesema kikosi chake kitaingia kambini rasmi Ijumaa ijayo, tayari kwa ajili ya kujiwinda na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Septemba 29, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkwasa alisema wamekuwa kimya kwa muda mrefu kutokana na kuendelea na usajili kwanza, lakini sasa suala hilo litakamilika wiki hii kabla ya Ijumaa ijayo kuingia kambini Mbweni, Dar es Salaam.

Kuhusu usajili mpya uliofanywa na timu hiyo, Nipashe lilimtafuta Ofisa Habari wa timu hiyo, Masau Bwire, ambaye alisema kila kitu kimekwenda vizuri na wanatarajia kutangaza nyota wao watakaunda kikosi hicho kabla ya kuingia kambini.

"Tayari tumeshapata mbadala wa vijana waliondoka, mashabiki wetu wawe na amani kwa sababu Ruvu Shooting haitoshikika msimu ujao," alisema Bwire huku akifafanua kuwa hawakuridhishwa na kumaliza nafasi ya 11 msimu uliopita na kwamba sasa malengo yao ni kuhakikisha wanapata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

Kuelekea msimu mpya, Ruvu Shooting imewapoteza wachezaji wake muhimu akiwamo Edward Manyama aliyehamia Azam FC, David Olomi aliyetimki Biashara United na Mohamed Banka 'Mo Banka' ambaye amejiunga na Namungo FC.

# SIMBA QUEENS YATAMBA KUTIKISA MBIO TIKETI YA CAF

**Na Somoe Ng'itu, NAIROBI**

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens, wametamba wataanza vizuri kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika watakapowakabili PVP FC kutoka Burundi katika mechi ya Kundi A, itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nyayo jijini hapa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali, alisema kikosi chake kimejipanga vema kusaka ushindi kuelekea mchezo huo na hana majeruhi hata mmoja.

Hababuu alisema wanaingia uwanjani wakiwaheshimu wapinzani wao kwa sababu wote ni mabingwa, hivyo hawatawabeza au kuwadharau.

Kocha huyo alisema wamejiandaa kukutana na ushindani kwa sababu kila timu imejiandaa kuonyesha kiwango kizuri na hatimaye kutumia malengo ya kupata tiketi ya kwenda kushiriki fainali za Afrika zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Misri.

"Haya ni mashindano ya Mabingwa wa kila nchi, na sisi ni mabingwa, hatutadharau mechi hata moja, hivyo tutapambana kuhakikisha tunapata tiketi ya kwenda Misri, kuipa heshima Simba na Tanzania, lakini pia kuweka rekodi," alisema Hababuu.

Kocha huyo alisema hali ya hewa ni nzuri na anaamini wachezaji wake wakifuata vema maelekezo waliyowapatia mazoezini, wataanza vizuri kampeni ya kusaka ubingwa wa michuano hiyo inayodhaminiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Nahodha wa Simba Queens, Violeth Nicholas, alisema wachezaji wote wako tayari kwa ajili ya kupeperusha vema bendera ya Tanzania na anafahamu hapa wamekuja kusaka ubingwa wa michuano hii.

"Kwetu kila mechi ni fainali, tumekuja vitani kupambana, tunaomba Mungu atusaidie kutimiza malengo yetu," alisema mchezaji huyo wa nafasi ya ulinzi.

Naye Mkuu wa Msafara wa timu hiyo, Asha Baraka alisema wamekuja Kenya kuchukua ubingwa ili kuendeleza desturi ya klabu yao katika kubeba mataji.

"Tumejipanga kufanya vizuri katika mashindano haya kwa sababu tunataka kumfurahisha na kumpa heshima Mama Samia Suluhu Hassan (Rais wa Tanzania," alisema Asha.

Bingwa wa michuano hii atauwakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), katika fainali zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Misri.

Mechi nyingine ya mapema ya Kundi A itakayochezwa kuanzia saa 8:00 itakuwa ni kati ya Mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Uganda, Lady Doves FC dhidi ya FAD kutoka Djibouti.



Wachezaji wa Simba Queens, wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Gymkhana Nairobi, Kenya kwa ajili ya kujiandaa na mechi dhidi ya PVP FC ya Burundi itakayochezwa katika Dimba la Nyayo leo. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Mtibwa itanirudisha Simba kwa kishindo - Ame*

**Na Tunu Hassan, TUDARCo**

LICHA ya kutua Mtibwa Sugar kwa mkopo, beki wa kati wa Simba, Ibrahim Ame, amesema kujiunga kwake na timu hiyo haina maana kwamba hana uwezo, bali hiyo ni fursa kwake kwenda kuonyesha kitu kingine tofauti kabla ya kurejea katika klabu yake kwa kishindo msimu ujao.

Akizumgumza na gazeti hili jana, Ame alisema anapenda kuipa thamani sehemu anayotoka, hivyo kutokana na uwezo aliokuwa nao ndani ya klabu ya Simba anakwenda kuudhihirisha.

"Naamini nitarudi Simba kutokana na uwezo nilionao, katika mechi zote nilizocheza nikiwa na klabu hiyo, naamini ni fundisho kwa watu wengine kwamba unaweza kucheza vizuri lakini bado ukawapisha watu wengine.

"Ninaweza kusema kwamba narudi Simba kwa sababu nitaenda kupata muda sana wa kucheza Mtibwa na nitaonyesha zaidi mimi ni nani na sikuwa Simba kwa kubahatisha tu, ila ni kwa sababu ya uwezo wangu,"alisema Ame.

Kuhusu suala zima la changamoto ya yeye kutolewa kwa kwa mkopo kwenda Mtibwa Sugar, Ame alisema suala hilo halikuwapo kabisa ila ni kwa mipango ya viongozi na yeye pia baada ya kuona hapati nafasi ya kucheza mara kwa mara akaona ni sawa kwake kuondoka kwa sasa.

"Unajua mnaweza kuwa wanne, lakini nafasi yangu ikawa duni, ila nilipokuwa napata nafasi nilikuwa naonyesha mimi ni Ame, Ame yule yule ambaye mmemzoea kumuona uwanjani akicheza mfululizo. Hiyo nikaona kila siku kukaa nje na uwezo nao unapungua kama mchezaji," alisema Ame

Nipashe lilipomuuliza haoni kwamba na yeye ni miongoni mwa wachezaji wazawa ambao wanaposajiliwa na timu kubwa huishia kuridhika na mishahara mikubwa pamoja na posho badala ya kuingia katika vita ya kupigania namba na nyota wakigeni na wengine, Ame alijiweka kando kwa kueleza yeye ni mpambanaji ila pengine ni mfumo tu wa kocha umemkataa.

"Hapana mpira siku zote ni kupata nafasi na tukirudi nyuma baada ya mimi kusajiliwa Simba nilikuwa nacheza chini ya Kocha Sven (Vandenbroeck), naamini watu wote waliona Ame ni nani, lakini mambo yakabadilika alipokuja kocha mpya (Didier Gomes) na mipango yake, tukaiheshimu akaamini watu wake, basi ndiyo ikawa hivyo. Hata ukiangalia mechi kama dhidi ya Namungo, Azam na Coastal Union, Ame ni yule Ame kweli," alisema.

# Michezo

Jumamosi Agosti 28, 2021

Nipashe


HABARI UK.22



## Jorginho, nyota Chelsea watawala tuzo Uefa

TUNAWASILI...

# YANGA: NJOONI KESHO MUONE UKUBWA WETU

### ●●● Mukoko aongoza nyota waliobaki Morocco kurejea, uongozi wasema kila kitu sasa kinaenda...

**Na Faustine Feliciane**

KUELEKEA Siku ya kilele cha Mwananchi, uongozi wa Klabu ya Yanga umewataka mashabiki na wanachama wao kufika kwa wingi Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho kujionea wenyewe maana halisi ya ukubwa wa klabu hiyo kwa kile watakachokionyesha.

Yanga kesho wanahitimisha Wiki ya Mwananchi kwa tamasha kubwa litakalofanyika uwanjani hapo litakaloambatana na kukata kiu ya mashabiki kwa utambulisho wa wachezaji wao kuelekea msimu mpya wa 2021/22 pamoja na mchezo wa kirafiki dhidi ya Zanzco FC ya Zambia.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM wanaodhamini timu hiyo, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili, Mhandisi Hersi Said, alisema kwa namna walivyofanya maandalizi tamasha hili litakuwa bora mara tatu ya lile lililofanyika mwaka jana.

**Alisema licha ya uwapo wa msemaji wao mpya, Haji Manara, bado na maandalizi waliyoyafanya yatachangia tamasha hilo kuwa kubwa zaidi.**

"Tumeanzia pale tulipoishia mwaka jana, kuna maboresho tumeyafanya na kuongeza burudani kwa ajili ya mashabiki na wanachama wa klabu yetu, lakini kikubwa ni namna tutakavyowatambulisha wachezaji wetu pamoja na 'sapraizi' nyingine," alisema Hersi.

Aidha, alisema kuwa mchezo wao wa kirafiki dhidi ya Zanaco utakuwa muhimu kwa kocha wao Nabi kuanza kukijaribu kikosi chake.

"Niwaambie tu Wanayanga, msimu huu tumekuja kivingine kuanzia kwenye tamasha letu la Wiki ya Mwananchi mpaka kwenye michuano ya Ligi Kuu, tunataka kuonyesha kweli ukubwa wa klabu yetu," aliongezea kusema Hersi.

Kilele hicho cha wiki ya Mwananchi kitapambwa kwa burudani mbalimbali kutoka kwa wasanii wa ndani huku pia mashabiki wakitarajia burudani kutoka kwa gwiji muziki wa dansi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Koffi Olomide.

Baadhi ya wachezaji wa kikosi cha Yanga walikuwa wamebaki nchini Morocco, akiwamo kiungo 'kisiki' Mukoko Tonombe, walitarajiwa kuwasili leo tayari kwa tamasha hilo na kisha kuendelea na mazoezi katika kambi ya timu hiyo Kigamboni, Dar es Salaam.

Yanga ambayo inajiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika, imefanya usajili mkubwa msimu huu ambapo kikosi chake kwa sasa kinaundwa na nyota watano kutoka DR Congo.



Kiungo wa Yanga, Mukoko Tonombe, muda mfupi kabla ya kukwea pipa kurejea nchini akitokea Morocco. **PICHA: YANGA.**

## Sababu Onyango kuachwa Harambee

**Na Somoe Ng'itu, NAIROBI**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Kenya ( Harambee Stars), Jacob Mulee 'Ghost', amefunguka sababu ya kumwacha beki wa Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Joash Onyango katika kikosi chake.

Septemba 2, mwaka huu Harambee Stars itawakaribisha Uganda (The Cranes), katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia wakati siku hiyo Tanzania (Taifa Stars), itakuwa ugenini dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa jana, Ghost alisema alimwacha beki huyo kwa sababu ni mgonjwa na atamhitaji katika mechi nyingine zinazofuata.

Ghost alisema Onyango bado ana kiwango cha juu na anamtegemea sana katika kuongoza safu ya ulinzi katika timu yake ambayo Septemba 7, mwaka huu itakuwa ugenini Kigali kuvaana na wenyeji, Rwanda (Amavubi).

"Onyango ni majeruhi, hata huko Morocco ambapo Simba imeenda kuweka kambi ya 'Pre Season' hajafanya mazoezi ipasavyo, niliwasiliana naye binafsi na kukubaliana nimpe muda wa kuona anapona kabisa," alisema kocha huyo wa zamani wa APR ya Rwanda na Tusker ya Kenya.

Aliongeza amefurahia kuona beki wake ametoa mchango mkubwa kwa Simba kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita na anaamini wataendelea kuiwakilisha vema Afrika Mashariki kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

"Wamewekeza na wameanza kujua umuhimu wa kusajili wachezaji wakubwa, mpira hauhitaji maneno, wachezaji wazuri wanaipa timu matokeo mazuri, ninawatakia heri katika mashindano ya msimu huu pia," aliongeza kocha huyo ambaye Yanga iliwahi kufanya naye mazungumzo ya kuinoa, lakini hakufanikiwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >